UCHANGANUZI WA MAKOSA YA KISARUFI KATIKA INSHA ZA WANAFUNZI WA GREDI YA SITA WA MTAALA WA UMILISI WA SHULE ZA MSINGI KATIKA GATUZI DOGO LA BUTULA BUSIA

OUMA EDMOND OKIYA

EDK/G/01-53876/2019

TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA TAALUMA YA ELIMU YA KISWAHILI, IDARA YA ELIMU YA LUGHA NA FASIHI CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA CHA MASINDE MULIRO

NOVEMBA 2025

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi tolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo chochote.

……..	**……..**
Sahihi	**Tarehe**
Okiya Edmond	**EDK/G/01-53876/2019**

IDHINI YA WASIMAMIZI

Tunayakinisha kuwa kazi hii ilifanywa na mtahiniwa kwa kuridhiwa nasi tukiwa wasimamizi wake.

…….. …….. ……. 06/11/ 2025….....
Sahihi Tarehe
Dkt. Frida Miruka
Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

....
Sahihi Tarehe
Dkt. Kang'ahi Maurine
Idara ya Mawasiliano Kielimu, Teknolojia na Masomo ya Mitaala
Chuo Kikuu cha Maseno,

IKISIRI

Lugha ya Kiswahili ina dhima muhimu katika jamii kwa hivyo changamoto zinazoikabili kwa vyovyote vile zinastahili kutatuliwa. Mojawapo ya changamoto hizi ni athari ya lugha ya kwanza kwa ujifunzaji wake. Hali hii huathiri wanafunzi kwenye viwango vyote vya elimu ikiwemo shule za msingi na hudhihirika kwa namna mbalimbali ikiwemo katika uandishi wa insha. Ukiukaji wa sheria za kisarufi za Kiswahili huchangia hali hii. Hivyo basi, Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi katika mtaala mpya wa elimu ya umilisi katika Gatuzi dogo la Butula. Madhumuni yalikuwa; kubainisha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa Kiswahili wa mtaala wa elimu ya umilisi, kuchunguza chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa Kiswahili wa mtaala wa elimu ya umilisi na kupendekeza mikakati ya kupunguza makosa ya

kisarufi katika insha za wanafunzi. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (NUM) ambayo iliasisiwa na Corder (1967), ambaye anasema kuwa kufanya kosa ni njia mojawapo ya kujifundisha lugha ya pili. Kwa hivyo, mwanafunzi anapofanya kosa, asiadhibiwe bali chanzo cha kosa kibainishwe. Muundo wa utafiti ulikuwa wa usoroveya elezi. Eneo la utafiti lilikuwa gatuzi dogo la Butula. Kundi lengwa lilikuwa wanafunzi 1100 wa gredi ya sita pamoja na walimu 72 wa Kiswahili wa shule 72 za msingi za kutwa. Mbinu za ukusanyaji data zilikuwa: uchunzaji, hojaji, usaili na uchanganuzi nyaraka. Vifaa vya utafiti vilivyotumiwa vilikuwa hojaji, orodha ya uchunzaji, mwongozo wa usaili na mwongozo wa uchanganuzi nyaraka. Sampuli za kimaksudi, kitabakishi na nasibu zilitumika. Usampulishaji kimaksudi ulitumika kuchagua shule 22 za msingi za kutwa na walimu 22 wa kiswahili. Usampulishaji kitabakishi ulitumika kugawa shule katika makundi huku usampulishaji nasibu ukitumika kuchagua wanafunzi 330 walioshiriki kwenye utafiti. Data ilichanganuliwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo na uchanganuzi wa kiidadi. Kipengele cha uchanganuzi kilikuwa matini zenye makosa ya kisarufi. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo katika aya, majedwali na chati. Matokeo ya utafiti yalibaini makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa mtaala wa umilisi kama ya kifonolojia (ubadilishaji wa sauti, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti, uyeyushaji). Makosa ya kimofolojia (kudondoa viambishi katika neno, kuunganisha na kutenganisha maneno visivyofaa). Makosa ya kisintaksia (upatanisho wa kisarufi katika sentensi). Makosa ya kisemantiki (matumizi ya msamiati usiofaa na mrundiko wa maneno katika sentensi). Chanzo cha makosa ya kisarufi yalitambuliwa kama: kutofahamu wakati wa kutumia sauti zingine, mielekeo ya wanafunzi, mbinu zisizofaa za ufundishaji miongoni mwa mengine. Matokeo yalionyesha kuwa makosa ya kisarufi yanaweza kutatuliwa kwa njia anuai kama: uhamasishaji wa wazazi kuhusu mfumo wa elimu ya umilisi, uandishi wa insha mara kwa mara, miongoni mwa mengine. Utafiti unahitimisha kuwa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa Kiswahili katika mtaala wa elimu ya umilisi gatuzi dogo la Butula ni mengi na yanajumuisha makosa ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Ingawa makosa mengi yametokana na athari ya lugha ya kwanza mengine yametokana na vyanzo mbalimbali. Mikakati mwafaka ikitumika kukabili tatizo hili, wanafunzi wataweza kuepuka makosa mengi. Uhamasishaji wa wazazi kuhusu elimu ya umilisi ni mojayapo ya mikakati mwafaka ya kurekebisha makosa haya. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, makosa ya kisarufi yalijitokeza katika insha za wanafunzi kisha vyanzo vyake kuchunguzwa, Mapendekezo yalitolewa ili kupunguza makosa haya kama vile Wizara ya Elimu kufuatilia na kuchunguza namna mwalimu anafundisha. Utafiti huu utawafaa washikadau wa elimu kama vile wanafunzi, walimu pamoja na maafisa wa elimu ili kubuni sera zinazofaa kuimarisha ufunzaji wa Kiswahili.

ABSTRACT

Kiswahili language performs a vital societal role hence the need to deal with the challenges that affect its use. One major challenge is first language interference on its learning and acquisition. This affects learners at all levels including primary or early grade learners and manifests in different ways including composition writing. One major cause of this is non observance of grammatical rules. Therefore, the aim of this study was to assess grammatical errors in Kiswahili compositions of grade six primary school pupils in the Competency Based Education (CBE) in Butula sub-County. The objectives of the study were; to identify grammatical errors of grade six Kiswahili pupils' composition in Butula sub-County; to asses the causes of grammatical errors of grade six Kiswahili pupils' compostions in Butula sub-County and to recommend possible

strategies to mitigate grammatical errors of grade six Kiswahili pupils' compositions in Butula Sub-County. The study employed a descriptive survey research design while being guided by the Error Analysis Theory propagated by Corder (1967) who asserts that errors are important in the learning process and can be used to understand how a language is learnt. He opines that it is important to identify the cause of an error instead of punishing the learners. The study was conducted in Butula Sub County. It targeted 1100 grade six pupils and 72 teachers of Kiswahili in 72 primary day schools. Data was collected through observation, questionnaire, interview and content analysis. The study employed purposive sampling to select 22 primary day schools and 22 grade six Kiswahili teachers, stratified sampling to categorise schools and simple randomn sampling to select 330 pupils who were involved in the research. Both qualitative and quantitative data analysis was conducted. The unit of analysis were texts with grammatical errors. The research findings were presented through essays in paragraphs, tables and charts. The findings indicated grammatical errors in pupils' composition including phonological errors like omission of sounds, omissions of syllables in a word, errors in word joining and separation. Morphological errors included syllable omission and erroneous joining and separation of words. Errors of grammatical alignment at sentence level and misuse of vocabulary at semantic level. The causes of grammatical errors were identified as ignorance on when to use certain sounds, students' attitude and poor teaching techniques. The study identified various strategies that could be used to mitigate errors as sensitization of parents on the CBE and regular composition writing exercises among others. The study concludes that grammatical errors are many and include phonological, morphological, syntactic and semantic errors. Although the main cause of error is mother tongue interference, there are other causes too. If proper strategies are employed, pupils will avoid such errors. Sensitisation of parents about CBE is a key strategy. The study recommends that the Ministry of Education takes charge to asses the teaching of composition in schools and how it is done. This study will be beneficial to various stakehoders like the students, teachers and education officers to enable them formulate relevant policies to develope and enhance the teaching of Kiswahili.

YALIYOMO

IKIRARI ……..…….……iii

IKISIRI …….……...…….....iv

ABSTRACT ……,,,.……v

MAELEZO YA DHANA xii

ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU xiii

SURA YA KWANZA 1

1.0 **UTANGULIZI** 1

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Suala la Utafiti 10

1.3 Madhumuni ya Utafiti 11

1.4 Maswali ya Utafiti 11

1.5 Umuhimu wa Utafiti 12

1.6 Misingi ya Uteuzi wa Mada 13

1.7 Upeo wa Utafiti 15

1.8 Muhtasari 16

SURA YA PILI 17

UHAKIKI WA MAANDISHI NA NADHARIA YA UTAFITI 17

2.0 Utangulizi 17

2.1 Nadharia ya Utafiti. 17

2.1.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (NUM) 17

2.1.2 Ufaafu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ……..……. 22

2.2 Aina za Makosa ya Kisarufi 23

2.2.1 Makosa ya Sarufi Sauti ……..……..23

2.2.2 Makosa ya Sarufi Maumbo ……..……...28

2.2.3 Makosa ya Sarufi Miundo ……..…….30

2.2.4 Makosa ya Sarufi Maana ……..……...31

2.3 Chanzo cha Makosa ya Kisarufi..... 32

2.4 Mikakati ya Kutatua Makosa ya Kisarufi 35

2.5 Muhtasari..... 39

SURA YA TATU 40

MUUNDO WA UTAFITI..... 40

3.0 Utangulizi..... 40

3.1 Muundo wa Utafiti 40

3.2 Eneo la Utafiti 41

3.3 Kundi Lengwa..... 41

3.4 Sampuli na Usampulishaji..... 41

3.5 Ukusanyaji wa Data 43

3.5.1 Mbinu za Ukusanyaji Data..... 43

3.5.1.1 Ujazaji wa Hojaji..... 43

3.5.1.2 Usaili 44

3.5.1.3 Uchunzaji 44

3.5.1.4 Uchanganuzi wa Nyaraka..... 45

3.5.2 Vifaa vya Ukusanyaji Data 45

3.5.2.1 Hojaji..... 45

3.5.2.2 Mwongozo wa Usaili 46

3.5.2.3 Orodha ya Uchunzaji..... 46

3.5.2.4 Mwongozo wa Uchanganuzi wa Nyaraka..... 47

3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data..... 47

3.7 Utegemevu na Uaminifu wa Data 49

3.8 Maadili ya Utafiti 49

3.9 Muhtasari..... 51

SURA YA NNE ...…….. .52

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA …… 52

4.0 Utangulizi ……... 52

4.1 Makosa ya Kisarufi ……..……. 52

4.1.1 Makosa ya sarufi sauti ….……..……..52

4.1.1.1 Udondoshaji wa Sauti …….……..... 53

4.1.1.1.1 Udondoshaji wa sauti /w/ …….……..53

4.1.1.1.2 Udondoshaji wa sauti /a/ ……..…… 54

4.1.1.1.3 Udondoshaji wa sauti /h/……... 55

4.1.1.1.4 Udondoshaji wa sauti /i/ ...……. 56

4.1.1.2 Makosa ya Uyeyushaji …..……..…….. 56

4.1.1.3 Uchopekaji wa Sauti ……..……... 57

4.1.1.3.1 Uchopekaji wa sauti /u/ …….. 58

4.1.1.3.2 Uchopekaji wa sauti /i/ ……... 58

4.1.1.4 Ubadilishaji wa Sauti …..…….. 59

4.1.1.4.1 Matumizi ya sauti /i/ badala ya /a/ ……..…60

4.1.1.4.2 Matumizi ya sauti /i/ badala ya /u/ …….……60

4.1.1.4.3 Matumizi ya sauti /y/ badala ya /l/ ……..…61

4.1.1.4.4 Matumizi ya sauti /y/ badala ya /w/ ……....62

4.1.1.4.5 Matumizi ya sauti /th/ badala ya /dh/ ……..62

4.1.2 Makosa ya Sarufi Maumbo ……..……64

4.1.2.1 Kutenganisha neno visivyo ……64

4.1.2.2 Kuunganisha maneno visivyo ……...…….65

4.1.2.3 Kuacha silabi katika neno ……..65

4.1.3 Makosa ya Sarufi Miundo ……..……..66

4.1.4 Makosa ya Sarufi Maana ……..……67

4.1.4.1 Matumizi ya msamiati usiofaa ……...67

4.1.4.2 Mrundiko wa maneno katika sentensi ……....68

4.2 Chanzo cha Makosa ya Kisarufi ……..……69

4.2.1 Kutofahamu wakati wa kutumia na kutotumia sauti /h/ ……...70

4.2.2 Athari ya lugha ya kimarachi ……71

4.2.3 Mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya kiswahili ……71

4.2.4 Mielekeo ya wanafunzi ……73

4.2.5 Maarifa na kutohitimu kwa walimu ……..74

4.2.6 Matumizi ya mbinu zisizofaa za ufundishaji ……75

4.2.7 Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia …….77

4.3 Hatua za Kutatua Makosa ya Kisarufi ……..…….....80

4.3.1 Uhamasishaji wa wazazi kuhusu mfumo wa elimu ya umilisi …….81

4.3.2 Uandishi wa insha …….81

4.3.3 Kutumia alama sahihi za usahihishaji wa insha ……82

4.3.4 Kubaini miundo tatanishi ……..83

4.3.5 Matumizi ya mbinu ya kutoa majibu ya moja kwa moja ……..85

4.4 Muhtasari ...……..85

SURA YA TANO ……..86

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ……..…….86

5.0 Utangulizi ..……..86

5.1 Muhtasari wa Matokeo ..……..86

5.1.1 Aina ya Makosa ya Kisarufi ..……..…….....86

5.1.2 Chanzo cha Makosa ya Kisarufi ……..…….87

5.1.3 Mikakati ya Kutatua Makosa ya Kisarufi ...……..……88

5.2 Mahitimisho …...……..89

5.3 Mapendekezo ya Utafiti ...……..…..……...89

5.4 Mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye ……...…….91

MAREJELEO..... 92

VIAMBATISHO …...……..…… 98

KIAMBATISHO I: HOJAJI YA WANAFUNZI ……...…….....102

KIAMBATISHO II: MWONGOZO WA USAILI WA WALIMU ……..….103

KIAMBATISHI III : MWONGOZO WA UCHUNZAJI ……...……..…....105

KIAMBATISHO IV: MWONGOZO WA INSHA YA WANAFUNZI ….…….. 105

KIAMBATISHO V: RAMANI YA KAUNTI YA BUSIA…….…….…….……...106

KIAMBATISHO VI: VIAMBATISHO VILIVYOJAZWA ..……....107

INSHA ZA WATAFITIWA ……..……..……...113

VIBALI VYA UTAFITI ……..……. 124

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1 : Udondoshaji wa sauti /w/ …….53

Jedwali 2 : Udondoshaji wa sauti /a/ ……. 54

Jedwali 3 : Udondoshaji wa sauti /h/ ……. 55

Jedwali 4 : Udondoshaji wa sauti /i/ …….. 56

Jedwali 5 : Uyeyushaji wa sauti /y/ na /w/ …… 56

Jedwali 6 : Uchopekaji wa sauti /u/ ……... 58

Jedwali 7 : Uchopekaji wa sauti /i/ …… 58

Jedwali 8 : Matumizi ya sauti /i/ badala ya /a/ ……... 60

Jedwali 9 : Matumizi ya sauti /i/ badala ya /u/ ……... 60

Jedwali 10 : Matumizi ya sauti /y/ badala ya /l/ …… 61

Jedwali 11 : Matumizi ya sauti /y/ badala ya /w/ ……... 62

Jedwali 12 : Matumizi ya sauti /th/ badala ya /dh/ ……..... 62

Jedwali 13 : Kutenganisha neno visivyo …… 64

Jedwali 14 : Kuunganisha neno visivyo ……..... 65

Jedwali 15 : Kuacha silabi katika neno …….. 65

Jedwali 16 : Makosa ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi …… 66

Jedwali 17 : Matumizi ya msamiati usiofaa ……... 67

Jedwali 18 : Mrundiko wa maneno katika sentensi ……... 68

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1 : Kutofahamu wakati wa kutumia na kutotumia sauti /h/ ……... 70

Kielelezo 2 : Mahali pa matumizi ya lugha ya Kiswahili ……..… 72

Kielelezo 3 : Mielekeo ya wanafunzi ……. 73

Kielelezo 4 : Maarifa ya kuhitimu na kutohitimu kwa walimu ……..… 75

Kielelezo 5 : Matumizi ya mbinu za ufundishaji ……... 76

Kielelezo 6 : Uwepo na matumizi ya vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji …….. 78

Kielelezo 7 : Matumizi ya lugha ya kwanza …….. 79

Kielelezo 8 : Mazoezi ya kuandika insha …….. 82

Kielelezo 9 : Mahali pa matumizi ya lugha ya kwanza …… 83

MAELEZO YA DHANA

Lugha ya Kwanza (L1)- Ni lugha ambayo mtoto hujifunza mara ya kwanza. Pia hurejelewa kama lugha asilia au lugha ya mama.

Lugha ya Pili (L2) - Ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kujifunza lugha yake ya kwanza.

Makosa - Ni kanuni ambazo zinakwenda kinyume na kanuni zilizowekwa zilizo sahihi.

Uchanganuzi Makosa - Ni mbinu itumiwayo kuthibitisha makosa yanayopatikana katika lugha anayojifunza mwanafunzi. Mbinu hii huchunguza aina ya makosa na visababishi vya makosa hayo. Ni njia ya kupambanua, kuainisha na kufafanua makosa yanayofanywa na mtu anayejifunza lugha ya pili.

Sarufi – Ni utaratibu wa kanuni ambazo humwezesha mtumiaji wa lugha kutunga tungo sahihi zinazoeleweka mara zinapotamkwa.

Insha - Ni kifungu cha maneno kilichopangwa kwa mpangilio maalumu wenye kueleza kuhusu jambo fulani uliopangwa katika aya.

Upataji Lugha – Ni uwezo wa binadanu kutumia lugha kwa kusikiliza, kusoma, kuandika na kuongea.

Ujifunzaji Lugha- Ni mchakato wa kupata ujuzi wa lugha mpya au kuboresha ujuzi wa lugha uliopo. Inahusisha kujifunza sarufi, msamiati, matamshi sahihi na uwezo wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika katika lugha hiyo.

Umilisi wa Lugha – Ni uwezo wa mzungumzaji kuwa na ufahamu fika kuhusu kanuni za kiisimu za lugha anayozungumza.

ORODHA YA VIFUPISHO NA AKRONIMU

L1	Lugha ya kwanza
L2	Lugha ya pili
KNEC	Kenya National Examination Council
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

SSK	Shule za wasichana za kutwa
SVK	Shule za wavulana za kutwa
SMK	Shule za mseto za kutwa
UM	Uchanganuzi Makosa
NUM	Nadharia ya Uchanganuzi Makosa
CBE	Competency Based Education

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Sura hii inafafanua usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, misingi ya uteuzi wa mada na upeo wa utafiti.

1.1 Usuli wa mada

Lugha ya Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kibantu (Mbaabu 1991; Chimerah 1998; Morgan 2024). Aidha ni Lingua Franka ya Afrika Mashariki na mojawapo ya masomo ya lazima kwenye mtaala wa elimu wa 8-4-4 na umilisi. Lugha ya kiswahili imesaidia kujenga stadi za lugha ambazo ni: kusikiliza, kuzungumza, kusoma na hata kuandika katika mawasiliano kwenye mtaala wa umilisi. Tume ya Mackay ya 1981 iliweza kunyanyua hadhi ya lugha hii kwa kuifanya kuwa somo la lazima katika shule za msingi, upili na vyuo vikuu. Fauka ya hayo, Katiba ya 2010 iliidhinisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi. Ili kutimiza malengo ya kitaifa ya elimu, lugha hii ni muhimu sana hivyo changamoto zinazoikabili kwa vyovyote vile zinastahili kutatuliwa. Mojawapo ya changamoto hizi ni athari ya lugha ya kwanza kwa ujifunzaji wake. Hivyo basi, Utafiti huu ulilenga kubainisha makosa ya kisarufi ambayo hujitokeza kwenye insha za wanafunzi wa shule za msingi katika mtaala mpya wa elimu ya umilisi katika Gatuzi dogo la Butula. Wanafunzi katika eneo la Gatuzi dogo la Butula hujifunza Kiswahili kama L2 yao huku L1 yao ikiwa Kimarachi ambayo ni lahaja ya Kiluhya. Kutokana na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili, lugha hii huweza kukumbwa na athari hasi (kuchopekwa na kudondoshwa kwa sauti katika maneno kimakosa.

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusiana na athari ya ujifunzaji wa lugha ya pili na makosa yanayotokana na athari hizi. Cross (2009) alifanya utafiti kwa wajifunzaji wa Kijapani ambao

hujifunza Kiingereza kama lugha ya pili. Matokeo kwenye utafiti wake yalitambua kuwa, wajifunzaji waliathiriwa na lugha yao ya kwanza. Wajifunzaji hao walitatizika kutofautisha herufi /b/ na /v/, walifanya makosa kuziunganisha herufi hizo mbili kwa kuzitamka kama /v/ ya Kijapani. Cross (2009) alijikita kwa kipengee cha fonolojia ilhali uatafiti huu umeangazia vipengele vyote vya sarufi. Kutokana na utafiti wake, kuna haja ya kushughulikia athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Utafiti huu uliangazia Lugha ya Kiswahili ambayo vitamkwa vyake ni tofauti na lugha ya Kiingereza.

He Dan (2010), katika utafiti wake alichanganua makosa ambayo hufanywa na wanafunzi wajifunzaji wa Kichina kwenye chuo kikuu cha Huizho, lugha yao ya kwanza ikiwa Kichina huku Kiingereza kama lugha yao ya pili. He Dan (keshatajwa) alihusisha Nadharia ya Mwingiliano Lugha kwenye utafiti wake ambapo aliangazia makosa yanayotokana na uhamishaji wa Kichina kwa Kiingereza. Sawa utafiti huu, He Dan (keshatajwa) katika utafiti wake alikusanya data kupitia insha za wanafunzi wa chuo kikuu tofauti na utafiti huu ambapo sampuli yetu ilikuwa wanafunzi wa shule ya msingi. Utafiti wake, ulifanywa China ilhali utafiti huu ulikitwa Kenya. Lugha ya pili ya watafitiwa ni Kiingereza tofauti na Kiswahili lugha iliyotafitiwa katika utafiti huu. Katika utafiti wake alitumia Nadharia ya Mwingiliano Lugha ilhali utafiti huu ulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Licha ya tofauti hizo, utafiti wake unaweza ukalinganishwa na wetu kwani tafiti zote mbili zinahusu kutafiti makosa kwenye lugha ya pili.

Kutokana na utafiti wa Gouala (1991), kuhusu athari za lugha asilia ya kwa lugha ya Kiingereza nchini Kongo kuhusu matamshi na muundo wa ripoti, wanafunzi huweza kukumbwa na matatizo kwenye matamshi na muundo wa lugha ya Kiingereza kutokana na lugha zao za asili. Hii inadhihirisha kuwa mwanafunzi huathirika na lugha asili katika uwezo wake wa kujifunza Kiingereza. Alitambua kwamba katika sehemu za mashambani lugha za asili zinatumiwa

kufundishia hadi darasa la mwisho la shule za msingi. Utafiti wa Gouala unatofautiana na utafiti huu kwa sababu, aliangazia athari za lugha asili kwa lugha ya Kiingereza ilhali utafiti huu ulizamia katika makosa ya kisarufi hasa vipengee vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki kwa wanafunzi wanaosoma katika shule za msingi. Isitoshe kwenye utafiti wake amezingatia lugha ya asili ya Kongo na Kiingereza ingawaje utafiti huu uliangazia lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha tofauti na inaathiriana kwa utofauti mkubwa.

Nchini Uganda, Haroon (1998), alishughulikia suala la kuathiriana kwa Kiswahili na Kigisu. Alitambua kuwa lugha ya Kigisu iliathiri mpangilio na muundo wa maneno katika sentensi za Kiswahili. Anaendelea kusema kuwa, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizi mbili, watafitiwa walifanya makosa ya kuhamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao kwa lugha ya pili (Kiswahili). Haroon (keshatajwa) aligundua kuwa hali hii ilikuwa chanzo cha makosa katika mpangilio wa maneno kwenye sentensi zilizotungwa na watafitiwa husika. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa sababu unafafanua vyanzo vingine vya makosa katika matini za wanafunzi. Kazi ya msomi huyu ni tofauti na ya utafiti huu kwa kuwa, mtafiti huyu alishughulikia kipengele cha sintaksia ilhali utafiti huu uliangazia vipengele vyote vya kisarufi.

Nchini Kenya Nga'ng'a (2002) alitafiti kuhusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili. Utafiti huo ulichunguza makosa ya kisarufi kwenye insha za wanafunzi wa darasa la saba na namna yalivyoshughulikiwa na walimu katika eneo la Ndaragwa nchini Kenya. Utafiti huo, ulishughulikia makosa ya kisemantiki, kisintaksia kimofolojia na kitahajia. Utafiti huu ni tofauti kwa sababu ulishughulikia makosa yote ya kisarufi ikiwemo makosa ya kifonolojia ambayo hayakushughulikiwa kwenye utafiti wa Ng'ang'a.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili TUKI (2013), wanafafanua sarufi kama mfumo taratibu na kanuni zinazotawala matamshi, maumbo, miundo na maana katika lugha. Wanaendelea kueleza kwamba taratibu na kanuni hizi ndizo humwezesha mzawa au mtumiaji yeyote wa lugha: 1) kutoa tungo sahihi zinazoeleweka, 2) kuelewa tungo ambazo zinatolewa na mtu anayetumia lugha hiyo. BAKITA, (2022) sarufi imefafanuliwa kama tawi la isimu ya lugha linaloangazia; fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia. Kwa hivyo, isimu katika lugha ni taaluma ambayo huchunguza na kuchambua mfumo na muundo wa lugha za binadamu. Fonolojia (sarufi sauti/matamshi) ni kipengele cha sarufi kinachochunguza na kuchambua utamkaji wa sauti za binadamu katika lugha husika na jinsi sauti hizo hutamkwa na mahali zinapotamkiwa sambamba na vipashio vyake. Mofolojia (sarufi maumbo) ni kipengele kinachojihusisha na maumbo ya maneno katika lugha. Sintaksia (sarufi miundo) huchunguza miundo na mpangilio wa maneno kwenye lugha. Nayo semantiki (sarufi maana) ni tawi la sarufi linalochunguza maana katika lugha za binadamu. Sawa na ufafanuzi wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala na Kamusi Kuu ya Kiswahili, Brinton (2000), anashadidia kuwa “sarufi katika taaluma ya lugha, hutumika kurejea kanuni au miongozo, ambayo hutawala lugha.” Kutokana na mtazamo huu, kwa hivyo sarufi ni kanuni, sheria au taratibu ambazo lugha husika hujipambanua. Matumizi ya lugha huongozwa na kanuni hizo. Kwa hivyo, sarufi inaweza kufasiliwa kuwa ni kanuni au taratibu ambazo zinatawala na kuongoza matumizi ya lugha husika. Kanuni hizo husika huweza kuwaongoza watumiaji wa lugha hiyo ili kutumia lugha kwa usahihi ikiwa ni pamoja na kutunga na kuunda tungo sahihi na zinazokubalika katika mfumo wa lugha ya jamii fulani.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2013) wanasema kuwa Sarufi ya Kiswahili ni mfumo wa taratibu na kanuni zinazotawala matumizi sahihi ya matamshi ya maneno, maumbo ya maneno, miundo ya tungo na maana ya miundo ya Kiswahili. Ni mfumo wa taratibu zinazomwezesha

mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili kutoa tungo sahihi za Kiswahili na pia zinazomwezesha mtu yeyote anayezungumza Kiswahili kuelewa tungo zinazotolewa na mtu mwingine anayetumia lugha ya Kiswahili. Nyangwine na wenzake (2010) wanasema kwamba Sarufi ya Kiswahili ni kanuni zinazotawala maumbo, matamshi, miundo na maana katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, sarufi ya Kiswahili, ni sarufi ambayo hujikita katika lugha ya Kiswahili. Ni taratibu na miongozo ya utumiaji wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na fasili ya sarufi ya Kiswahili, ni wazi kabisa kuwa sarufi ya lugha ya Kiswahili huwasaidia wazungumzaji wa lugha hii kutambua miundo sahihi ya sentensi wanazozitunga na maneno wanayoyaunda; kuelewa tungo zinazotungwa na watumiaji wengine wa lugha ya Kiswahili.

Sarufi ya Kiswahili imegawanyika katika viwango (tanzu) vikuu vinne ambavyo ni: sarufi matamshi, sarufi maumbo, sarufi miundo na sarufi maana.

Kwanza, Sarufi sauti au matamshi(fonolojia). Kwa mujibu wa Kadeghe (2012), sarufi matamshi huchambua vitamkwa (fonimu) vya lugha inayohusika, ikionesha namna na mahali kila kitamkwa kinapotamkwa. Neno ‘vitamkwa’ (kikiwa kimoja ni ‘kitamkwa’) kulingana na kamusi kuu ya Kiswahili limetumika kumaanisha sauti zinazotamkwa katika lugha fulani. Naye Matinde (2012), anasema sarufi matamshi ina wajibu wa kuchunguza na kufafanua sauti za lugha na uamilifu wake katika mfumo mahususi. Anachokisema Matinde hapa, ni kwamba kazi kubwa ya sarufi matamshi ni kuchunguza na kutoa ufafanuzi kuhusu utendaji kazi wa sauti za binadamu katika lugha maalumu. Hivyo basi, sarufi matamshi ni kiwango au kipengele cha sarufi kinachohusika na uchunguzi pamoja na uchambuzi wa sauti za lugha mahususi. Sauti za lugha mahususi ina maana kuwa ni sauti za lugha fulani kama Kiswahili, Kingoni, Kisukuma, Kinyarwanda, Kichina. Zinakuwa sauti maalumu au mahususi pale zinapobainishwa kuwa ni sauti za lugha fulani kama mifano iliyotajwa hapa. Sarufi matamshi ya Kiswahili huchunguza sauti za binadamu na utendaji

kazi wake katika lugha ya Kiswahili – yaani, huchunguza uamilifu wa sauti za lugha ya Kiswahili. Aidha, inachunguza na kubainisha sifa za sauti, uamilifu wake na jinsi sauti hizo zinavyotamkwa na kuambatana katika kuunda vipashio vikubwa zaidi ya fonimu; huchunguza namna na mahali sauti hutamkiwa.

Pili, Sarufi Maumbo, Massamba (2016) inatoa fasili ya sarufi maumbo kuwa ni "tawi la isimu (*maana ya isimu imefafanuliwa, rejea maana ya sarufi*) ambalo huchunguza maneno na aina za maneno." Hiki ni kiwango au kipengele cha sarufi ambacho hujikita katika uchunguzi wa maumbo ya maneno kwa kuzingatia uchunguzi wa miundo (jinsi maneno yanavyoundwa) ya maneno, makundi ya maneno na uhusiano wa maneno pamoja na taratibu za uundaji wa maneno. Sarufi maumbo ya Kiswahili huchunguza na kuchambua maumbo ya maneno ya Kiswahili, na namna maumbo hayo yanavyotumika kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili pamoja na maana au dhana zinazowakilishwa na maumbo hayo. Tawi hili la sarufi, hushughulikia uchunguzi na uainishaji wa vipashio vya kimaumbo kama mofu na alomofu zake, viambishi, mzizi, shina pamoja na uamilifu wa vipashio hivyo sambamba na mofimu za vipashio hivyo (maana zinazobebwa na vipashio vilivyotajwa). Huchunguza pia uainishaji wa aina za maneno kwa kuzingatia kigezo cha kimaumbo, kimuundo na kimaana.

Tatu, Sarufi Miundo. Hiki ni kiwango cha sarufi kinachojulikana pia kama sintaksia. Massamba na wenzie (2012) wanaeleza kuwa sarufi miundo ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Nao TUKI (2013) wanafasili sarufi miundo kuwa ni tawi la isimu (sarufi) linaloshughulikia uchanganuzi wa mpangilio na uhusiano wa vipashio katika kila sentensi. Fasili za wataalam hawa zikichunguzwa kwa umakini zinabainisha kitu kimoja au kilekile. Hii ni wazi kuwa sarufi miundo ni sarufi

inayoshughulikia miundo ya tungo katika lugha. Huchunguza mpangilio wa tungo katika lugha ya binadamu na jinsi mpangilio huo unavyoweza kudokeza maana au dhana iliyolengwa na iliyo sahihi. Sarufi miundo ya Kiswahili hujikita kwenye kuchunguza na kuchambua miundo ya tungo za Kiswahili. Kwa maana hiyo, sarufi miundo si kitu kingine bali ni kipengele cha sarufi chenye kujikita katika uchunguzi, uchambuzi na ufafanuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Fauka ya hayo, katika tawi hili la sarufi kinachochunguzwa ni zile sheria au kanuni ambazo ni lazima zifuatwe katika kupanga maneno ya lugha katika mfuatano kwa namna ambayo inafanya maneno hayo kuleta maana inayokubalika na kueleweka katika lugha fulani. Huchunguza tungo kama neno inavyoweza kuungana na tungo neno kuunda tungo kirai au tungo kishazi hadi sentensi sanjari na kuchunguza viambajengo vinavyounda tungo hizi.

Nne, Sarufi Maana (Semantiki). Wanaisimu Habwe na Karanja (2004) wanafafanua sarufi maana kuwa ni utanzu wa sarufi unaochunguza maana katika lugha ya mwanadamu. Vilevile, Mekacha (2011) anaeleza kuwa semantiki ni taaluma inayochanganua na kufafanua miundo na mifumo ya maana na kipashio chake cha msingi katika uchanganuzi ni leksimu, umbo lenye maana moja. Kwa maana hiyo basi, ni dhahiri kuwa sarufi maana ni kipengele cha sarufi kinachochunguza na kuchambua maana katika lugha za binadamu. Sarufi maana ya Kiswahili huchunguza na kuchambua maana zinazokuwa zimebebwa na tungo katika lugha ya Kiswahili. Maana zinazochunguzwa kwenye kiwango hiki cha sarufi ni zile maana za maneno, vifungu vya maneno (kirai na kishazi) na sentensi. Hapa ndipo wanasarufi (isimu) huchunguza na kuchambua nadharia mbalimbali zinazofasili maana, aina za maana, jinsi ufasili wa watumiaji wa lugha huathiri maana katika lugha.

Ilikuwa muhimu kufanya utafiti wa aina hii katika lugha ya Kiswahili ili kuchunguza namna viwango vya sarufi za lugha hii zilivyotumika na hata mpangilio wake katika insha za wanafunzi wa shule za msingi Gatuzi dogo la Butula.

Insha ni mojawapo ya vipengele vya somo la Kiswahili ambapo hutahini ubunifu wa mwanafunzi na umilisi wa sheria za lugha ya Kiswahili. Sanja na Kusino (2006) wanadai kuwa insha ni mtungo unaoandikwa kwa mfululizo au kinathari na unaozungumzia mada fulani. Insha ni sehemu muhimu katika mtihani wa Kiswahili katika shule za msingi na sekondari kulingana na silabasi ya Kiswahili ya mtaala wa 8-4-4. Insha ni mojayapo ya vipengee vya somo la Kiswahili. Mwanafunzi huhitaji kuandika insha moja ya alama ishirini. Mwanafunzi kuandika insha anahitaji kuwa mbunifu na afuate sheria na kanuni za lugha ya Kiswahili. Uandishi mzuri hutokana na mwanafunzi kuelewa sheria za lugha ambazo zimo katika lugha husika na jinsi mwanafunzi anavyozitumia kanuni hizi kisarufi na kimsamiati ili kuibuka na insha inayowasilisha ujumbe kwa njia inayotarajiwa. Utafiti huu ulilenga kuchanganua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi.

Kulingana na ratiba ya mtaala mpya wa elimu ya umilisi nchini Kenya, mfumo wa umilisi wa 6-3-3-4 ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka wa 2017 ukichukua nafasi ya mfumo wa 8-4-4. Mitihani ya kitaifa katika shule za msingi inastahili kufanywa na wanafunzi wa gredi ya pili, nne na sita. Katika mtaala huu wa elimu ya umilisi wazazi wanahusika kwa njia moja au nyingine katika kusaidia watoto kufunzwa shuleni na walimu, hasa kusaidia kukuza talanta za wanao. Mtaala wa elimu ya umilisi umewapa wazazi nafasi ya kuwasaidia wanafunzi katika kuandika insha kupitia mitagusano yao, ingawa wazazi wengi katika sehemu za mashambani kama vile sehemu kubwa ya Gatuzi dogo la Butula hawana umilisi wa uandishi wa insha. Kupitia kwa mitagusano baina ya wazazi na wanafunzi husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa na kuandikwa visivyo. Mtaala huu umeleta mabadiliko

makubwa sana katika ufunzaji na ujifunzaji wa masomo kumi na mbili katika shule za msingi ambayo yanastahili kufunzwa kwa njia ya utendaji. Mtaala wa elimu ya umilisi unawahitaji wanafunzi watumie asilimia kubwa ya muda uliotengewa somo wakijifunza kwa vitendo wakiwa pamoja.

Ufunzaji wa Kiswahili katika mtaala mpya wa elimu ya umilisi katika shule za msingi unaegemea jinsi mwanafunzi anakitumia Kiswahili katika mawasiliano, maandishi na kutatua changamoto za maisha. Hii ni tofauti na katika mtaala wa awali wa 8-4-4 ambapo mwanafunzi anajifunza Kiswahili kwa minajili ya mitihani. Katika mtaala wa elimu ya umilisi wazazi wana mchango katika mafunzo ya wanao kando na kulipa karo. Wazazi wanashirikishwa katika mafunzo ya wanao ilihali hawakuhamasishwa na serikali kuhusu huu mtaala wa elimu ya umilisi. Lugha za asili zimeungwa mkono kimatumizi katika mtaala wa elimu ya umilisi, hii ni kwa sababu lugha za asili zinatarajiwa kuimarisha lugha ya Kiswahili lakini hali hii sio jinsi ilivyo.

Gatuzi dogo la Butula linapatikana katika Gatuzi la Busia nchini Kenya. Wakaazi wa eneo hili ni wamarachi lugha yao ya utagusano ikiwa Kimarachi mojawapo ya lahaja za Kiluhya ambayo ni miongoni mwa lugha za kibantu. Kutokana na utandawazi na uhamiaji baadhi ya wamarachi wamehamia mijini na sehemu zingine za nchi. Lahaja ya Kimarachi ndiyo lugha ya wenyeji wa Gatuzi dogo la Butula na baadhi ya sehemu za Gatuzi dogo la Nambale kulingana na ripoti ya idara ya sensa (2019). Kuna maingiliano na maathiriano kati ya lugha ya wanafunzi wazawa wa kaunti ndogo ya Butula na Kiswahili. Lugha asilia ya wanafunzi wengi wa shule za msingi katika Gatuzi dogo la Butula wanaojifunza Kiswahili ni Kimarachi. Kwa hivyo Kimarachi kama lugha asili inakubalika kimatumizi kutokana na mtaala wa elimu ya umilisi. Maathiriano na matumizi ya lugha ya Kimarachi katika mtaala wa elimu ya umilisi imesababisha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi. Hali hii ilituwezesha kuchanganua makosa hayo ya

kisarufi katika insha za wanafunzi wa Kiswahili wa shule za msingi katika mtaala mpya wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula. Basi kunalo tatizo la utafiti ambalo lastahili kutafitiwa kudhihirisha makosa ya kisarufi kutokana na maingiliano na maathiriano ya lugha ya wazawa wa Gatuzi dogo la Butula na lugha ya Kiswahili.

1.2 Suala la utafiti

Lugha ya Kiswahili ina asili yake katika lugha za kibantu (Guthrie 1971). Kwa hivyo inahusiana na lugha nyingine za Kibantu katika vipengele mbalimbali ikiwemo sarufi. Kimarachi ni mfano wa lugha za Kibantu inayozungumzwa katika Gatuzi dogo la Butula. Kwa vile Kiswahili ni lugha ya kibantu pamoja na hali kwamba lugha asilia imepewa kipaumbele katika mtaala wa umilisi, inatarajiwa kuwa wakaazi wa eneo hili wawe na ujuzi mwafaka wa Kiswahili na kuitumia ipasavyo. Kwa hivyo wanafunzi wa gredi ya sita wa shule za msingi Gatuzi dogo la Butula wanatarajiwa kuwa na ujuzi wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo kinyume cha hali hii kimeshuhudiwa. Lugha ya Kiswahili ni muhimu na ina mawanda mapana kimatumizi, tofauti na lugha zingine za Kibantu. Lakini pamoja na umuhimu wake huo mkubwa, lugha hii imekumbwa na changamoto kwa wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili. Kwenye mtaala wa elimu ya umilisi kuna msisitizo wa lugha ya asili ambayo inatarajiwa kuinuwa hadhi ya lugha ya Kiswahili lakini lugha hiyo asili imesababisha changamoto ya makosa ya kisarufi kwa lugha ya Kiswahili. Palikuwa na haja ya kutafiti na kutambua makosa ya kisarufi yanayojitokeza katika insha za wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi ili kupendekeza njia ambazo walimu wanaweza kuwasaidia wanafunzi ili kuimarisha lugha ya Kiswahili. Utafiti huu basi ulilenga kuchunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi ambayo huenda yanachangiwa na mtagusano baina ya lugha asili ya Kimarachi na Kiswahili katika Gatuzi dogo la Butula.

1.3 Madhumuni ya utafiti

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi. Azma ikawa ni kupendekeza mikakati ya kupunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi katika Gatuzi dogo la Butula. Ili kufikia lengo hili madhumuni yafuatayo yaliangaziwa;

1. Kubainisha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa somo la Kiswahili wa shule za msingi katika mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula.
2. Kuchunguza chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa somo la Kiswahili wa shule za msingi katika mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula.
3. Kupendekeza mikakati ya kutatua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa somo la Kiswahili wa shule za msingi katika mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula.

1.4 Maswali ya utafiti

1. Ni makosa gani ya kisarufi ambayo hudhihirika katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa somo la Kiswahili wa shule za msingi katika mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula?
2. Nini chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa somo la Kiswahili wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula?
3. Ni mikakati ipi inayoweza kutumiwa kuyakabili makosa ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa gredi ya sita wa somo la Kiswahili wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula?

1.5 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu ni wa manufaa kwani utawasaidia washikadau wa elimu kama vile wanafunzi, walimu na maafisa wa elimu kuwa na uelewa wa makosa ya kisarufi katika ujifunzaji wa Kiswahili na hivyo kuwasaidia kutambua sababu za kutokea kwa makosa haya wakati wa kujifunza na kufundisha Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu yatawafaa walimu watakaoyarejelea ili kutabiri uwezekano wa kutokea kwa makosa wakati wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi na kujua jinsi ya kukabiliana na makosa haya.

Isitoshe, kupitia kwa utafiti huu, wanafunzi na walimu wataweza kutambua mbinu na njia mwafaka za kufuata ili kusuluhisha makosa haya, njia za utatuzi wa makosa haya zikizingatiwa kutokana na jinsi utafiti huu uliziainisha kutakuwepo na utamkaji na uandishi wa Kiswahili sanifu.

Katika ngazi za elimu, utafiti huu utakuwa muhimu kwa waundaji sera na mitaala ya elimu kwa kuwa wanapotunga mitaala ya elimu ya Kiswahili watazingatia mikakati iliyopendekezwa katika utafiti huu (uhamasishaji wa wazazi kuhusu mfumo wa elimu ya umilisi, uandishi wa insha mara kwa mara, kutumia alama sahihi za usahihishaji wa insha, kubaini miundo tatanishi na matumizi ya mbinu ya kutoa majibu ya moja kwa moja). Utafiti huu utawafaa waundaji mtaala wa elimu ya umilisi namna ya kuboresha ufunzaji wa Kiswahili.

Utafiti huu pia utakuwa na mchango katika kusisitiza nafasi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa. Ikumbukwe kuwa ni lugha yenye kanuni zake zinazostahili kuzingatiwa katika matumizi yake ya kila siku.

Utafiti huu utakuwa kichocheo cha tafiti nyingine kuhusu mtaala wa elimu ya umilisi vilevile kuhusu kuathiriana kwa matamshi ya lugha asilia na Kiswahili katika jamii za Kenya na hata za nje ya nchi. Hivyo, utasaidia kuweka wazi njia nyingine mbalimbali za kuwasaidia wazawa wa lugha fulani katika kujifunza Kiswahili. Tena utakuwa rejea mojawapo kwa tafiti nyingine kuhusu elimu ya Kiswahili.

1.6 Misingi ya uteuzi wa mada

Ni bora kuboresha matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa mtaala wa elimu ya umilisi. Pana haja ya kushughulikia makosa ya kisarufi katika Kiswahili kwa kuwa uchanganuzi wa makosa hayo utasaidia katika harakati za kujaribu kuyarekebisha makosa ya kimatamshi na kimaandishi miongoni mwa wanafunzi.

Kiswahili ni lugha muhimu kwa kuwa ina majukumu mengi katika nchi. Zaidi ya kuwa ni lugha inayotumiwa katika mawanda mapana kama vile siasa, utawala na biashara miongoni mwa mengine, pia ni lugha inayowaunganisha wanajamii mbalimbali kwa kuwa hutumiwa na wazungumzaji ambao lugha zao za kwanza ni tofauti. Pia Kiswahili ni mojawapo kati ya masomo ambayo hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa.

Licha ya matokeo duni katika somo la Kiswahili katika shule za msingi, tafiti nyingi zilizofanywa kama vile katika ripoti ya Musau (2018) zinaegemea sana namna ujifunzaji wa Kiswahili unaathirika kutokanana mbinu za ufundishaji na ufunzaji wa Kiswahili. Katika mtaala wa elimu ya umilisi mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni tofauti kwani mwanafunzi ndiye anastahili kutoa suluhisho kando na mtaala wa awali ambapo ufundishaji uliegemea sana mwalimu.

Ujifunzaji wa Kiswahili pia umekumbwa na changamoto kama inavyodhihirika katika ripoti ya Musau (2018) kama Kiswahili kupewa vipindi chache kwenye ratiba ya masomo. Katika mtaala

wa elimu ya umilisi vipindi vya Kiswahili vimepunguzwa kutoka saba hadi vinne. Pia Shule za msingi, ambazo asilimia zaidi ya 80 ni shule za kutwa zinasajili matokeo duni kwa mujibu wa ripoti ya KNEC (2019). Naye Kimaro (makala katika gazeti la Nation, Machi 21, 2013) alilalama kuwa matokeo ya Kiswahili yalikuwa ya chini mno. Sababu alizotoa zilikuwa pamoja na: utopa katika silabasi ya Kiswahili, upungufu wa walimu, Kiswahili kutengewa muda mchache ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza miongoni mwa sababu nyigine. Kunazo sababu za kiisimu na zisizo za kiisimu ambazo huchangia matokeo duni, utafiti huu utatupatia mwanga katika swala hili. Ingawa sampuli ilitoka katika Gatuzi dogo la Butula Gatuzi la Busia, matokeo yake yanaweza kujumlishwa katika jamii nzima. Athari za matamshi ya lugha ya kwanza ni mojawapo inayochangia matokeo duni katika Kiswahili katika Shule za msingi za kutwa katika Gatuzi dogo la Butula. Sababu ni kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wa shule za kutwa ni wenyeji wa eneo la shule, vilevile hutumia lugha ya uzawa ya Kimarachi katika mtagusano wao nyumbani na hata shuleni iwapo hamna sera ya udhibiti lugha.

Insha ni kipengee ambacho kinadhihirisha umilisi katika lugha ya Kiswahili hasa kuonyesha umilisi kwa njia ya kuandika. Huwa ni mojayapo ya karatasi mbili ambazo hutahiniwa katika mtihani, kwa hivyo ina mchango mkubwa kwa matokeo ya mtihani wa kitaifa wa mwanafunzi. Mwanafunzi anapofanya makosa katika insha yake humpelekea kupata matokeo duni katika mtihani wake kwa hivyo makosa yanastahili kudhibitiwa ili kuboresha matokeo. Ingawaje katika mtaala wa elimu ya umilisi hakuna kuweka wanafunzi katika viwango, kila mwanafunzi huandika insha kulingana na uwezo wake.

Licha ya Wizara ya Elimu kutoa mwelekeo na mafunzo kuhusu mtaala mpya wa elimu ya umilisi kwa walimu, wengi wao wangali wanatatizika jinsi ya kuendeleza mafunzo hayo kwa wanafunzi Wanto Warui (Machi 10, 2020). Mtaala wa elimu ya umilisi una mchango mkubwa wa kuyafikia

na kuyatimiza malengo ya elimu. Elimu ya utendaji ndiyo inayosisitizwa kwenye mtaala huu. Kiswahili ni mojawapo ya masomo kumi na mbili katika mtaala huu ambapo mwanafunzi anastahili kujifunza Kiswahili lugha na insha katika somo la kiswahili. Kwa hivyo mwanafunzi pamoja na mwalimu akiwa na changamoto kwa upande wa kuelewa mtaala huu itakuwa vigumu kuyafikia malengo ya elimu ya nchi.

1.7 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulichunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa Kiswahili wa shule za msingi wanaotumia mtaala wa elimu ya umilisi. Utafiti huu ulifanyika katika Gatuzi dogo la Butula katika Gatuzi la Busia, Kenya. Ulijikita tu kwa shule za msingi za kutwa zilizo katika Gatuzi dogo la Butula kwa sababu huko ndiko kuna wazungumzaji karibu wote wa lugha ya Kimarachi kama lugha yao ya kwanza L1. Kundi wakilishi lilikuwa wanafunzi wa gredi ya sita kutoka shule lengwa.

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili shule za msingi Gatuzi dogo la Butula.

Utafiti huu ulishughulikia vipengele vinne vya kisarufi: fonolojia (sarufi sauti), mofolojia (sarufi maumbo), sintaksia (sarufi miundo) na semantiki (sarufi maana).

Utafiti huu ulihusisha madhumuni yafuatayo; Kubainisha makosa ya kisarufi yanayodhihirika kwenye insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi, Kueleza chanzo cha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi, Kupendekeza mikakati ya kupunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi.

Uchunguzi huu ulihusisha wanafunzi wa gredi ya sita na walimu wa somo la Kiswahili wala sio somo lingine. Vilevile ulijikita tu kwa insha za wanafunzi pekee, kipengee cha sarufi ndicho kilichoangaziwa kwenye utafiti huu.

1.8 Muhtasari

Sehemu hii imeshughulikia usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, upeo na tahadhania za utafiti.

SURA YA PILI

UHAKIKI WA MAANDISHI NA NADHARIA YA UTAFITI

2.0 Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha tahakiki ya maandishi kuhusiana na mada ya utafiti, inafafanua nadharia ya utafiti, aina za makosa ya kisarufi, chanzo cha makosa ya kisarufi na mikakati ya kutatua makosa ya kisarufi.

2.1 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadhari ya Uchanganuzi Makosa ili kubainisha makosa yanayojitokeza katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wanaojifunza Kiswahili wa mtaala wa elimu ya umilisi wa shule za msingi katika Gatuzi dogo la Butula na kuelezea vyanzo vya makosa hayo.

2.1.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa (NUM)

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliasisiwa na Corder (1967) baada ya kugunduliwa kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi isingetegemewa katika kubashiri kiwango kikubwa cha makosa yaliyotokea katika lugha. Huu ni mtazamo ambao haukuweza kubashiri ugumu uliodhihirika katika ujifunzaji wa lugha. Nadharia hii ya Uchanganuzi Linganuzi ilitumiwa sana kati ya miaka ya 1940 na 1960 ambapo ulinganuzi wa lugha mbili mahususi ulitumiwa kama msingi wa kuchanganua makosa yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wale waliokuwa wakijifunza lugha ya pili. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa Inashikilia kuwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hufanya makosa ambayo yanaweza kubainishwa, kuchambuliwa, kuainishwa na kutathminiwa ili kubainisha mfumo unaofanya kazi. Nadharia hii huweza kutumia mbinu ambazo ni za kiisimu katika kuangazia makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha.

Inaelekeza ni kwa jinsi gani makosa hayo yanavyoweza kushughulikiwa. Lado (1957) anaeleza kwamba makosa yanayofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili yanatokana na maingiliano ya lugha ya kwanza ilhali Corder (1967) anaeleza kwamba makosa mengi ya wajifunzaji wa lugha ya pili yanatokana na wajifunzaji wenyewe kutumia kimakosa kanuni za lugha ya pili wanayojifunza. Mwalimu ana uwezo wa kuainisha makosa haya pale ambapo anaelewa ule mfumo wa lugha ya kwanza ya mwanafunzi.

Nadharia hii inachunguza makosa kwa kuyahusisha na vyanzo mbalimbali na uhamishaji hasi kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Inaelezea kimakundi makosa yanayofanywa na wale wanaojifunza lugha ya pili huku ikifichua hali ya wanafunzi kukiuka kaida kupitia kwa ufasiri potovu wa vipengele fulani vya lugha na miundo.

Kisakwah (2014) akimnukuu Larsen (1992) anasema nadharia ya uchanganuzi makosa huchunguza idadi ya makosa ya wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili. Makosa hayo huwa sio yale yanayosababishwa na athari ya lugha ya kwanza pekee bali pia yale makosa ya kijumla. Kulingana na Larsen (keshatajwa), makosa huweza kuwekwa katika vitengo kadhaa vikiwemo; ujumlishaji mno wa kiholela, matumizi ya sheria zisizo toshelezi, kutozingatia kanuni za lugha husika na ubunifu wa fikra zisizo za kweli.

Selinker (1972) na Richard (1974) wameorodhesha aina nne za makosa katika tungo kama ifuatavyo; uhamishaji lugha, ufundishaji mbaya wa lugha ya pili, mikakati ya kuwasiliana katika lugha ya pili na ujumlishaji mno wa kiholela.

Uhamishaji-lugha ni utaratibu wa kuhamisha kiambajengo cha lugha moja na kukitumia katika lugha nyingine. Wanafunzi wengi haswa huchukulia kuwa sheria za lugha ya kwanza na za lugha

ya pili zinafanana. Wanafunzi hujua kuwa, kanuni zinazotawala lugha mbili ni sawa kwa hivyo zinaweza kutumiwa katika lugha zote mbili kwa njia ya kubadilishana.

Ufundishaji mbaya wa lugha ya pili ni hali ambayo hutokana na ukosefu wa umilisi wa lugha ya pili. Mwalimu hukosa mbinu mwafaka anapofunza lugha ya pili. Mwalimu hukosa ujuzi toshelezi katika lugha kwa kuwa baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa zikiwemo ujumlishaji wa kiholela na pia matumizi mabaya ya sheria za lugha husika.

Mikakati ya kuwasiliana katika lugha ya pili hutokana na njia mahususi ambazo watu hujifunza ili kuweza kuwasiliana na wazungumzaji asilia wa lugha lengwa. Mara kadhaa, mwanafunzi hujaribu kadri awezavyo ili akabiliane na upungufu alionao katika lugha lengwa. Kwa sababu hiyo mwanafunzi huyo hujikakamua ili afikie mawasiliano bora iwezekanavyo.

Ujumlishaji mno wa kiholela ni utoaji wa maelezo ya kijumla sana hadi kuvuka mpaka. Wanafunzi aghalabu hutumia sheria kiholela au hata pasipofaa. Kwa hivyo kutokana na harakati hizo, wanafunzi hubuni ruwaza kuhusu lugha lengwa na pia kuzitumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Hali hiyo hutatiza matumizi ya lugha ya pili na vilevile kusababisha makosa mengi katika lugha ya pili.

Elis (1997) anasema kuwa, makosa husababishwa na kutozingatia sheria za lugha, na ikiwa mwanafunzi ana uwezo wa kukosoa kosa lake yeye binafsi, basi hilo halifai kushughulikiwa. Anasisitiza kwamba, ikiwa mzungumzaji ana uwezo wa kushughulikia makosa yake katika lugha na kuyarekebisha vilivyo basi hali hiyo inaashiria kuwa mzungumzaji ana umilisi wa lugha hiyo. Hali kadhalika, ikiwa mzungumzaji hana uwezo wa kukosoa kosa lake basi hilo ni kosa ambalo linafaa kushughulikiwa vilivyo kwa kuwa mzungumzaji huyo hana umilisi wa lugha na hatambui sheria zozote za lugha husika.

Nadharia ya uchanganuzi makosa inajumuisha seti za kanuni zinazotumiwa kuyatambua, kuyakinisha na kufafanua makosa ya wanafunzi katika maandishi na uzungumzaji wa lugha ya pili. Pia inaeleza ni jinsi gani makosa yanaweza kushughulikiwa. Nadharia hii inasisitiza mbinu za kuichunguza lugha ya mwanafunzi. Katika nadharia hii makosa huchukuliwa kama ishara kuwa mwanafunzi anajaribu kujifunza na kuelewa mfumo wa lugha lengwa. Kwa hivyo, nadharia hii inampatia mwanafunzi nafasi ya kutosha katika ujifunzaji kwa kuchunguza makosa anayoyafanya katika ujifunzaji wake.

Inaelekeza ni kwa jinsi gani makosa ya wanafunzi yanavyoweza kushughulikiwa. Nadharia hii inadai kuwa baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili hutokana na athari ya lugha ya kwanza. Makosa hayo yanaweza kuainishwa kulingana na kiwango cha lugha na kwa hivyo kuna makosa kama vile ya kifonolojia, kimsamiati au kileksia, kisintaksia na kimofolojia. Aidha, makosa hayo yanaweza kuchunguzwa kulingana na kiasi kinachoweza kutatiza mawasiliano. Kuna yale yanaweza na yale yasiyoweza kukwamisha mawasiliano.

Mwasisi wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, anapendekeza hatua zifuatazo katika kuchanganua makosa ambazo pia ndiyo mihimili ya nadharia hii; (Coder, 1974; Al-khresheh, 2016)

i. Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha.
ii. Kutambua makosa
iii. Kufafanua makosa. Makosa yanawekwa katika makundi na kuelezwa kisarufi. Makosa yenyewe ndiyo hutumiwa katika kuainisha kategoria za kisarufi.
iv. Kufafanua vyanzo vya makosa ya kisarufi.
v. Kutathmini makosa. Kuyasahihisha makosa haya ili kujua jinsi ya kukabiliana nayo.

Sridhar (1981) naye anazitambua daraja nane zifuatazo katika Nadharia ya Uchanganuzi Makosa:

i. Ukusanyaji wa data

ii. Utambuaji wa makosa yenyewe

iii. Uainishaji wa makosa mbalimbali

iv. Kuonyesha idadi ya kila kikundi cha makosa yaliyoainishwa

v. Utambuaji wa vipengele vinavyosababisha matatizo katika lugha ya pili

vi. Urekebishaji wa makosa

vii. Kuchanganua vyanzo vya makosa

viii. Kuonyesha athari inayosababishwa na tokeo la kosa

Norish (1983) anaeleza kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaweza kutumiwa kutoa picha ya aina ya matatizo yanayowakumba wanafunzi. Anaandika kwamba utafiti huo ukifanywa kwa ukamilifu unaweza kusaidia katika uandishi wa miongozo ya masomo. Anasisitiza kuwa nadharia hii hutoa mwangaza kuhusu mbinu anazotumia mwanafunzi ili kuepuka matatizo hayo ya ujifunzaji wa lugha ya pili.

Maoni yaliyotolewa na wataalamu, Corder (1974), Sridhar (1981) na Al-khresheh (2016) yalitufaidi katika utafiti huu haswa katika hatua za uchanganuzi makosa. Kulingana na maoni ya wataalamu hao; kazi zilizoandikwa na wanafunzi hukusanywa, makosa hutambuliwa kwa kupigiwa msitari. Makosa hayo huainishwa na kuwekwa katika makundi mbalimbali kama vile makosa ya kifonolojia, ya kimofolojia, ya kisintaksia na ya kisemantiki. Makosa hayo hutafutiwa visababishi vyake kama vile tafsiri ya moja kwa moja, ujumlishaji mno na uhamishaji. Makosa hayo husahihishwa kisha kurekebishwa kwa kuonyesha majibu yanayostahili kwenye kitabu cha

mwanafunzi. Kwa kuzingatia haya, mwanafunzi anapoipitia kazi iliyosahihishwa na kutambua makosa aliyoyafanya na majibu yaliyostahili, ataweza kuepuka makosa hayo katika kazi zitakazofuatia. Hata mwalimu atakapoipitia kazi hiyo darasani ataweza kumwelezea mwanafunzi visababishi vya makosa yake na kwa hivyo kurekebisha makosa hayo.

2.1.2 Ufaafu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia hii katika kubainisha aina za makosa ya kisarufi yanayodhihirika kwenye insha za wanafunzi wanaotumia mtaala mpya wa elimu ya umilisi katika Gatuzi dogo la Butula. Makosa haya yalitambuliwa kutoka kwa data iliyokusanywa. Nadharia hii ilitufaa ili kuchunguza vyanzo vya aina mbalimbali za makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi katika Gatuzi dogo la Butula. Ambapo baadhi ya makosa yalikuwa na zaidi ya chanzo kimoja hii ni kutokana na maoni ya Larsen (1992). Baada ya nadharia hii kutuongoza kutathmini makosa katika insha za wanafunzi, utafiti ulizua mbinu za kuyarekebisha makosa tuliyotambua kutokana na data tuliyokusanya. Hatua hii ilitufaa kwa kutoa mwelekeo kwa washikadau mbalimbali katika viwango mbalimbali kuhusu mbinu mwafaka za kurekebisha makosa yaliyotokea katika matini za watafitiwa na kupunguza utokeaji wa makosa yenyewe. Hii ilifanyika ili kuboresha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika shule za msingi.

Nguzo za nadharia ambazo zilitumika katika kuchanganua madhumuni ya utafiti huu ni; kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha, kutambua makosa, kufafanua makosa ambapo makosa yanawekwa katika makundi na kuelezwa kisarufi makosa yenyewe ndiyo hutumiwa katika kuainisha kategoria za kisarufi, kufafanua vyanzo vya makosa hayo na kutathmini makosa kwa kuyasahihisha makosa haya ili kujua jinsi ya kukabiliana nayo.

2.2 Aina za Makosa ya Kisarufi

Kutokana na kuathiriana kwa lugha mbili tofauti huweza kuzua utata wa matamshi na maandishi katika lugha ya pili. Kila lugha huwa na mfumo fulani wa sauti mahususi ambao unastahili kufuatwa. Mfumo huo usipozingatiwa husababisha makosa katika mazungumzo na maandishi kama vile insha za wanafunzi. Makosa yalijitokeza katika vipengee vinne vya kisarufi.

2.2.1 Makosa ya sarufi sauti (kifonolojia)

Makosa ya sarufi sauti yalihusisha udondoshaji wa sauti. Nyagah (2016) ameonyesha udondoshaji katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa kimeru. Ameonyesha jinsi sauti huachwa katika maandishi wakati fonimu mbili zinapokaribiana na kusababisha makosa. Vipashio hudondoshwa katika silabi, neno, kirai au kishazi na kusababisha makosa kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo: Udondoshaji wa sauti /h/, kama vile; *akuna badala ya hakuna, *asubui badala ya asubuhi na*uko badala ya huko. Udondoshaji wa nazali /n/; *dugu badala ya ndugu na*walikujwa badala ya walikunjwa. Udondoshaji wa nazali /m/; *matebezi badala ya matembezi na*nikakubuka badala ya nikakumbuka.

Kuna pia makosa ya uchopekaji wa sauti. Nyagah (keshatajwa) ameonyesha uchopekaji katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wa kimeru. Nyagah (keshatajwa) ameonyesha namna sauti za irabu, konsonanti na kiyeyusho huchopekwa katika neno katika mazingira ambapo sauti hizo hazistahili na kusababisha kutokea kwa makosa kama ifuatavyo: Uchopekaji wa sauti /h/ kama vile *habiria badala ya abiria na *hile badala ya ile. Uchopekaji wa irabu /u/ kama vile *mutu badala ya mtu na *munene badala ya mnene. Uchopekaji wa irabu /i/ kama vile *asikari badala ya askari na *alishituka badala ya alishtuka.

Utumiaji mbadala wa sauti, ni mbinu ambapo sauti ambayo haipatikani katika mfumo wa lugha fulani inabadilishwa na sauti nyingine au sauti inayokaribiana nayo. Mchakato huu ulichangia makosa katika kazi ya Nyagah (2016) kama ifuatavyo; Matumizi ya sauti /s/ badala ya /z/ kama vile *kupotesa badala ya kupoteza na *ulisa badala ya uliza, Matumizi ya /s/ badala /sh/ kama vile *mastaka badala ya mashtaka na *suka badala ya shuka, Matumizi ya sauti /g/ badala ya /gh/ kama vile *gala badala ya ghala na *gafla badala ya ghafla, Kuchanganya matumizi ya sauti /th/ na /dh/ kama vile *walithoofika badala ya walidhoofika na *thambi badala ya dhambi.

Kulingana na Akoth (2014), kuna pia uchanganuzi makosa na muundo wa sentensi. Anasema kwamba kila lugha huwa na mfumo fulani wa sauti mahususi ambao unastahili kufuatwa. Kwa hivyo, kutozingatiwa kwa mfumo huo ndio husababisha makosa mengi katika tungo za wanafunzi. Katika tasnifu yake alionyesha makosa ya kisarufi ambayo yalidhihirika katika insha za wanafunzi wa Kisuba kama vile udondoshaji na uchopekaji wa sauti. Amefafanua udondoshaji kuwa ni utaratibu wa kukitoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au kishazi ilhali uchopekaji ni uingizaji wa irabu, kiyeyusho au konsonanti katika neno fulani. Mifano ya makosa ya kisarufi kutoka kwa data yake yanayohusu udondoshaji na uchopekaji wa sauti ni kama vile: *Ana badala ya hana na *Aribu badala ya haribu. Akoth (keshatajwa) kwenye tasnifu yake ametambua makosa ya matumizi mabaya ya sauti, katika insha za wanafunzi alitambua matumizi ya sauti /s/ badala ya /sh/ kama vile katika neno *samba badala ya shamba.

Mashaka (2015) anaeleza kuwa makosa ya kisarufi huathiri matamshi au sauti za lugha mahususi. Kutokana na utafiti wake wa fonolojia ya lugha ya Kijita na Kiswahili aligundua kuwa lugha hizi mbili zinaingiliana pakubwa. Kuingiliana huku husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo. Anafafanua kwamba mwanafunzi anapohamisha sauti aliyoizoea katika lugha yake ya kwanza kwenda katika lugha ya

Kiswahili kwa njia isiyofaa basi mwanafunzi huyo atakuwa amefanya makosa. Mashaka (2015) kwenye tasnifu yake aligundua kuwa wanafunzi hutatizika kwa sababu sauti walizozizoea katika lugha ya Kijita hazipatikani katika lugha ya Kiswahili au zile zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili hazipatikani katika lugha ya Kijita. Baadhi ya makosa ya kifonolojia ni kama yafuatayo.

Wanafunzi wa Kijita walifanya makosa ya kudondosha sauti /h/ katika baadhi ya maneno na kupata miundo isiyofa kama vile *ajaenda badala ya hajaenda. Matumizi ya sauti mbadala; baadhi ya wanafunzi walibadilisha sauti kwa njia isiyostahili na kusababisha makosa kama vile; matumizi ya /z/ badala ya /dh/ *zarau badala ya dharau. Matumizi ya /s/ badala /th/ *salasini badala ya thelathini. Matumizi ya /r/ badala ya /l/ *mshare badala ya mshale. Matumizi ya /bh/ badala ya /b/ *bharidi badala ya baridi.

Obara (2014) anasema kuwa maingiliano baina ya lugha ya Ekegusi na Kiswahili husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo. Makosa haya hutokea wakati mwanafunzi anapohamisha sauti aliyoizoea katika lugha yake ya kwanza kwenda lugha ya Kiswahili. Wakati mwingine wao huchanganya matumizi ya sauti kwa sababu ya kuathirika na lugha ya kwanza. Makosa ya kisarufi ambayo Obara. (keshatajwa) alitambua ni:

Matumizi mbadala ya sauti. Wanafunzi wengi hukanganya wasijue jinsi ya kutumia baadhi ya sauti mbili ipasavyo zinazokaribiana kimatamshi. Mwanafunzi anapojifunza Kiswahili inamlazimu kujifunza sauti isiyopatikana katika lugha yake ya kwanza kama vile /l/. Matatizo hutokea wakati sauti aliyoizoea mwanafunzi katika lugha yake ya kwanza huwa haipatikani katika lugha ya Kiswahili. Hivyo mwanafunzi atatamka iliyo karibu nayo. Kama vile matumizi ya /r/ badala ya /l/ *nikienderea badala ya nikiendelea. Matumizi ya /ch/ badala ya /j/ *sichui badala ya

sijui. Matumizi ya /s/ badala ya /z/ *msee badala mzee. Matumizi ya /s/ badala ya /sh/ *nilisikwa badala ya nilishikwa. Matumizi ya /p/ badala ya /b/ *ameniipia badala ya ameniibia.

Amos (2019) kwenye tasnifu yake alitambua makosa ya mageuzi ya vokali kama vile udondoshaji wa vokali yanayofanywa na wanafunzi katika uandishi wa insha. Alionyesha kuwa mchakato wa udondoshaji hutokea pale ambapo vokali inapatikana kati ya konsonanti mbili au mwishoni mwa neno baada ya konsonanti. Kama vile vokali /i/ ilidondoshwa katika mazingira ya katikati ya konsonanti mbili na baada ya konsonanti; *asubuh badala ya asubuhi, *mahakaman badala ya mahakamani. Vokali /a/ ilidondoshwa mwishoni mwa neno kama vile; *aliend badala ya alienda, *napend badala ya napenda. Irabu /e/ ilidondoshwa katikati ya maneno kama vile *nimenda badala ya nimeenda, *amendesha badala ya ameendesha.

Ubadala wa vokali ni makosa ambayo yalidhihirika katika insha za wanafunzi wa Kisomali katika kazi ya Amos (keshatajwa). Alionyesha kuwa vokali nyingi zilitumiwa kwa kubadilishwa na vokali nyingine kama vile matumizi ya irabu /e/ badala ya /i/ katika maneno *hevyo badala ya hivyo na *mwesho badala ya mwisho. Matumizi ya irabu /o/ badala ya /u/ kama vile maneno *rodi badala ya rudi, *shole badala ya shule. Kwa upande mwingine makosa ya mageuzi ya konsonanti pia yalishughulikiwa na Amos (keshatajwa) katika tasnifu yake kwa wanafunzi wa kisomali wanaojifunza Kiswahili. Mageuzi ya konsonanti yalidhihirika katika michakato mbalimbali ya kifonolojia kama vile; Uchopekaji wa konsonanti /j/ katika neno *ongeya badala ya ongea, *anasomeya badala ya anasomea. Uchopekaji wa /n/ kama vile *rundi badala ya rudi, *mafunta badala ya mafuta. Wanafunzi wa kisomali walifanya makosa ya ubadala wa konsonanti /k/ badala ya /g/ kama vile *zanku badala ya zangu, *yanku badala ya yangu. Ubadala wa /f/ badala ya /v/ kama vile *fita badala ya vita, *futa badala ya vuta. Makosa ya kudhoofika kwa irabu na konsonanti yalifanywa na wanafunzi katika insha katika kazi ya Amos (keshatajwa). Anasema

kuwa makosa ya kudhoofika kwa sauti yanatokea wakati sauti fulani inayopatikana katika lugha Kiswahili inageuzwa na kuwa sauti tofauti na wanafunzi wa Kisomali kama vile; *kuanza badala ya kwanza na *kuea badala ya kwea.

Makosa ya uchopekaji wa sauti na matumizi mbadala ya sauti yalidhihirika katika kazi za wanafunzi kutokana na tasnifu ya Otiende (2013). Kutokana na utafiti wake kuhusu fonolojia ya Kiswahili na Kiolusuba aligundua kuwa kuna tofauti kati ya miundo ya maneno fulani. Tofauti hizo huathiri matumizi ya Kiswahili kwa kiwango fulani kimatamshi na kimaandishi ambayo husababisha wanafunzi kufanya makosa kama vile; makosa ya uchopekaji wa irabu /u/ mfano *mutu badala ya mtu, *mugeni badala ya mgeni. Makosa mengine yanayotambuliwa na Otiende (keshatajwa) ni matumizi mbadala ya sauti /s/ badala ya /ɵ/ kama vile; *asari badala ya athari, *semanini badala ya themanini. Anaendelea kusema kuwa mfumo wa fonimu wa Kiolusuba hauna sauti /ɵ/. Kwa hivyo mzungumzaji ambaye anazungumza Kiolusuba kama L1 anapoitumia Kiswahili anaishia kudhihirisha athari za sauti nyingine katika kuitamka sauti hii hali ambapo inampelekea kufanya makosa.

Wairimu (2016) ameonyesha makosa ya kisarufi wanafunzi wa Kiamu wanaojifunza Kiswahili hufanya katika kazi zao andishi. Katika utafiti wake alitambua kuwa wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa lahaja ya Kiamu kama lugha yao ya kwanza wanapojifunza Kiswahili sanifu hufanya makosa mbalimbali ya kifonolojia kama vile; Matumizi mbadala ya sauti; sauti /y/ badala ya /j/ *yua badala ya jua, *pamoya badala ya pamoja. Matumizi ya /z/ badala ya /v/ *ziatu badala ya viatu, *ziazi badala ya viazi. Matumizi ya /d/ badala ya /z/ *kwanda badala ya kwanza, *fundwa badala ya funzwa. Makosa ya udondoshaji wa sauti katika kazi andishi pia yalitambuliwa katika kazi ya Wairimu (keshatajwa). Anasema kuwa wanafunzi wa Kiamu wanapoandika baadhi ya maneno huacha sauti fulani nje hali ambapo husababisha makosa ya kifonolojia katika Kiswahili.

Kama vile udondoshaji wa sauti /l/ *kueta badala ya kuleta, *mbee badala ya mbele. Kutokana na utafiti wake Wairimu (2016), mara nyingi wanafunzi wa Kiamu wanaojifunza Kiswahili hudondosha konsonanti /l/ katika baadhi ya maneno inapotokea katikati ya irabu mbili. Hivyo wanafunzi wanapohamisha sifa hii ya kudondosha konsonanti katika maneno iwapo inatokea katikati ya irabu mbili katika kuandika insha za Kiswahili sanifu inadhihirika kuwa ni makosa.

2.2.2 Makosa ya Sarufi Maumbo

Tafiti mbalimbali zimebainisha makosa ya sarufi maumbo. Ontieri (2015) anabainisha udondoshaji kama hali ya kuondoa kipashio katika mofu kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Udondoshaji ni tendo la kutoa kipashio fulani cha kiisimu kutoka mfumo maalumu katika silabi, neno, kirai au kishazi (TUKI 2013 na Massamba 2007). Udondoshaji wa vipashio unaweza kufanyika katika sentensi kwa kuondoa neno, maneno au kifungu fulani cha maneno. Kwa mujibu wa Ontieri (keshatajwa) kosa la udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa njia ambayo inakiuka taratibu za lugha husika. Katika makala tafitiwa kosa la udondoshaji lilifanyika wakati mofu /a/ ilidondolewa katika neno “atajiunga” na kuandikwa -tajiunga, /i/ ikadondolewa katika neno “hatima” na kuandikwa “hatma’

Makosa ya uchopekaji yalijitokeza katika kazi ya Massamba (2007) ambaye alieleza uchopekaji kama hali ya uingizaji wa kitamkwa mwanzoni, ndani au mwishoni mwa neno. Hivyo, uchopekaji ni kitendo cha kuingiza au kuchopeka kipashio kwenye vipashio vingine. Uchopekaji unaweza kuwa ni wa kuingiza kitamkwa, mofu au neno katika mlolongo wa vipashio. Mofu /w/ huchopekwa katika neno “hatujamchagua” na kuwa *hatujamchaguwa, mofu /u/ huchopekwa katika neno “msataafu” na kuwa *mustaafu.

Kulingana na utafiti wa Nyagah (2016), baadhi ya wanafunzi hutumia maneno ya lugha yao ya kwanza wakidhani kuwa mfanano wa kimaumbo huwa sawa na mfanano wa kimaana jambo ambalo husababisha utata wa kimaana au upotoshi wa maana. Katika kazi yake ilionekana kwamba wanafunzi walitumia maneno yenye miundo sawa au inayokaribiana na ile ya Kiswahili sanifu wakidhani kuwa maana yake ni sawa. Kwa mfano, mwanafunzi anapoandika, "Dereva alituma gari lianguke" kitenzi *tuma* kinazua utata na hata maana iliyokusudiwa kupotea kwani tunabaki kujiuliza, tangu lini gari likawa na uwezo wa kutumwa? Vivyo hivyo mwanafunzi anapoandika, "Niliitikia kuandamana nao hadi hospitalini", kitenzi *itikia* kinaleta dhana tofauti kabisa katika Kiswahili. Baadhi ya maumbo yaliyotumiwa na wanafunzi yalikuwa ya maneno ya kategoria tofauti, hivi kwamba dhana zilizowakilishwa na maumbo hayo zilikuwa tofauti vilevile.

Kemunto (2017), anaeleza katika kazi yake kwamba wanafunzi wengi hutatizwa na maneno yaliyo marefu sana kiasi cha kufikiria kuyatenganisha ili yawe mawili au zaidi. Asemavyo Mbaabu (1995), umbo la neno la aina hiyo huwa na mzizi wa vitenzi. Kabla ya mzizi huo viungo kadha wa kadha kama vile viambishi, na viungo vya wakati hutumiwa. Baada ya mzizi viambishi vya kauli au jinsi tofauti kama vile –***ewa***- (kutendewa), -***esha*** (kutendesha) na -***ana-*** (kutendana) hupachikwa kwa mzizi wa kitenzi. Kwa kuwa viungo hivyo vyote havipatikani vikiwa huru, vyote pamoja na mzizi wa kitenzi huunda neno moja. Hivyo basi, neno moja linapotenganishwa hapatakuwepo na mawasiliano. Baadhi ya maneno yafuatayo yalitenganishwa kutokana na utafiti wa Kemunto (keshatajwa), *huji nufaisha, *ita kusanyika, *zitakazo wawe zesha, *mwana funzi.

Lugha ya Kiswahili ina mofimu mbalimbali ambazo huunganishwa kwa kuunda maneno ya Kiswahili kama anavyodai Kemunto (keshatajwa). Maneno haya huwa ya aina mbalimbali, kwa mfano, nomino, Kivumishi, kitenzi, kielezi, kiwakilishi, kiunganishi, kihusishi na kihisishi. Kila neno lazima lijisimamie katika sentensi kulingana na uhitaji. Kwa sababu hii kuunganishwa kwa

maneno husababisha utata katika sentensi ya Kiswahili. Asemavyo Mbaabu (1995), maneno mawili yanapounganishwa huunda istilahi mpya za Kiswahili ambazo hutumiwa katika maandishi pasi kujua kama zinawasilisha maana au la. Kemunto (2017), aligundua kwamba wanafunzi waliyaunganisha maneno kiholela katika kazi andishi hali ambayo ilisababisha makosa ya kisarufi na kuvuruga maaana iliyokusudiwa kupitishwa. Maneno yaliyounganishwa kimakosa ni kama vile: *ilikuwawezesha, *anasifanjema, *nizamuhimu.

2.2.3 Makosa ya Sarufi Miundo

Makosa ya sarufi miundo ni sawa na makosa ya upatanisho wa kisarufi. Upatanisho wa kisarufi ni utaratibu wa kimuundo ambapo nomino huwakilishwa na vipashio vingine vinavyohusiana nayo katika tungo. Upatanisho huleta uwiano au ukubalifu katika tungo kati ya nomino kiima na vipashio vingine vinavyoambatana nayo kwenye tungo ili kuleta mantiki na maana inayoeleweka (Mdee na wenzake 2013, TATAKI 2013, Baraza la Kiswahili la Taifa [BAKITA] 2022). Bila upatanisho wa kisarufi mantiki katika tungo hukosekana. Kwa maana hiyo kosa la upatanisho wa kisarufi ni hali ya kuweka vipashio visivyoleta mantiki au maana inayoeleweka katika tungo husika. Kama vile sentensi, (*msemaji huo ameweza) badala ya msemaji huyo ameweza. (*Sanamu la kike lilitumika) badala ya sanamu wa kike alitumika.

Umoja na wingi ni dhana za kisarufi zinazodokeza idadi. Dhana hizi kiisimu humilikiwa na kategoria ya kisarufi ijulikanayo kama idadi (Habwe na Karanja 2004; Matinde 2012). Umoja humaanisha kuwa kitu, hali au jambo ni moja wala si zaidi ya hapo ila wingi humaanisha kuwa ni zaidi ya moja. Katika uwanja wa isimu umoja na wingi huhusu nomino na hudhihirishwa kwa viambishi vya ngeli na upatanisho wake Matinde (ameshatajwa), katika utafiti wake wanafunzi

waliandika (wanane walifika kwao) badala ya nane walifika kwao. (maofisi yao ni ile) badala ya ofisi yao ni ile.

2.2.4 Makosa ya sarufi maana

Uchunguzi wa Mushumbwa (2020) ulibaini uwapo wa kosa la mpangilio wa vipashio usiotakiwa katika tungo. Kemunto na Ontieri (2018) wanasisitiza kuwa katika tungo maneno yanastahili kupangwa kwa njia ambayo inaweza kuleta maana kamili na ukiukwaji wake husababisha ujumbe kuvurugika. Vilevile, wanasisitiza kuwa si kila mpangilio wa maneno unaoleta maana kamili ni sahihi kwa kila lugha. Katika Lugha ya Kiswahili, inawezekana kabisa mpangilio wa vipashio ukaleta maana ila usiwe sahihi au haukubaliki. Hivyo maneno huweza kuwa na maana yanaposimama pekee lakini yakakosa kuwa na maana katika tungo. Kama vile (langu jina ni Amina) badala ya jina langu ni Amina, (amekuja mtoto) badala ya mtoto amekuja. Tungo hizi hazina mpangilio sahihi wa vipashio katika Kiswahili. Mpangilio bora huanza na nomino kisha kitenzi. (S=N + T) au (S =N +V + T +E). Yaani nomino huweza kufuatwa na kitenzi au kivumishi kisha kitenzi na iwapo kuna kielezi.

Akoth (2014) aligundua kwamba wanafunzi huhamisha misamiati kutoka lugha yao ya kwanza na kuitumia katika lugha ya pili. Wanafunzi wanaposhindwa kupata msamiati mwafaka katika Kiswahili wao huamua kutumia msamiati wa lugha ya kwanza ili kukidhi mahitaji yao ya lugha ya pili. Wanafunzi wanapofanya hivi huifanya sentensi kukosa kuwa na maana ya ujumbe uliokusudiwa. Mfano (Hamisi alikunywa sigara) badala ya Hamisi alivuta sigara (Waungaji wa timu ya Gor Mahia walisafiri. Badala ya mashabiki wa timu ya Gor Mahia walisafiri.

Maoni na tafiti za wataalamu waliotafiti kuhusu aina za makosa za kisarufi yalikuwa kichocheo katika utafiti wetu. Utafiti huu ulihusisha kazi zao kwa kutambua na kubainisha aina za makosa

ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula.

2.3 Chanzo cha Makosa ya Kisarufi

Mojawapo ya vyanzo vya makosa ya upatanisho wa kisarufi ni Ujumlishaji, Norrish (1983) anasema kuwa ujumlishaji unatokana na tajiriba ya mwanafunzi katika matumizi yake ya L2 ambapo anatunga tungo zenye makosa kwa kujumuisha kanuni za L2. Katika hali hii wanafunzi hutatizwa na sauti zingine zinazokiuka utaratibu wa kawaida wa upatanisho wa kisarufi. Nyagah (2016) ametolea mfano wa makosa ya udondoshaji na uchopekaji wa sauti /h/ ambamo haimo katika mfumo sauti wa Kitigania. Kwa hivyo wanafunzi walichanganyikiwa ni wakati upi sauti hii inafaa kutumiwa na ni lini haifai. Selinker (1972) anaeleza kuwa makosa haya yanatokana na ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa katika lugha kati. Kwa hivyo, kwa kuwa lugha ya Kiswahili huwa na sauti /h/ wanafunzi huishia kuitumia kiholela inapotanguliwa na irabu. Hali hii inatokana na juhudi za wanafunzi kurahisisha miundo ya lugha lengwa kama mkakati wa mawasiliano. Hata hivyo usahilishaji huu hujitokeza tu katika udondoshaji wa /h/ kwani utamkaji wa irabu pekee kama silabi huwa rahisi ikilinganishwa na utamkaji wa silabi ya konsonanti /h/ na irabu.

Kuna baadhi ya makosa yanayofanywa na wajifunzaji lugha ya Kiswahili ambayo hutokana na ufundishwaji usiofaa, hivi kwamba wanafunzi wamerithishwa makosa na walimu wao jambo ambalo linakuwa gumu kwao kulifahamu. Selinker (keshatajwa) anawalaumu walimu wanaofundisha lugha ya pili. Anasema kuwa, wengi wao hawana umilisi wa lugha ya pili na pia baadhi yao hutumia mbinu zisizofaa wanapofunza lugha ya pili. Walimu wanapotumia mbinu zisizofaa katika ufundishaji husababisha wanafunzi kufanya makosa katika kazi zao.

Ntawiyanga (2015) anasema kuwa katika mahojiano yake na walimu wa Kiswahili, ilibainika kuwa wanafunzi walifanya makosa kwa kuwa shule zao hazikuwa na walimu wa kutosha waliohitimu masomo yao katika lugha ya Kiswahili. Hali hii ndiyo iliyowafanya baadhi ya wanafunzi waunde vipashio vyenye makosa kama *huyu ndi, huyu ndimi, huyu ndiko, (shamba) wamba, (shamba) limba, (shamba) amba*. Uchunguzi wa data hii ulionyesha kuwa wanafunzi waliofanya makosa haya hawakuwa na taarifa yoyote kuhusu miundo sahihi iliyotarajiwa kutolewa. Makosa hayo yanatokana na ufundishaji usiofaa kwa kuwa walimu wao hawana uelewa mwafaka kuhusu Kiswahili. Ufundishaji na ujifunzaji wa L2 ni tofauti na ufundishaji wa kawaida kwa sababu huhitaji maarifa, ujuzi na umilisi wa L2 inayofundishwa. Aidha, wafundishaji wanatakiwa wawe wamepitia mafunzo maalumu ambayo huwawezesha kuwafundisha wajifunzaji kwa kutumia stadi na mbinu mbalimbali ili waweze kufikia umilisi wa L2. Utafiti huu ulichunguza iwapo kuna ufundishaji usiofaa kupitia kwa kutambua makosa ya matumizi ya sauti mbadala zitakazojitokeza katika insha za wanafunzi wa Kiswahili.

Kwa mujibu wa Sarah (2018), shule nyingi za kata hasa zilizo vijijini sana zina upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu. Mara nyingi vitabu ambavyo hupatikana katika shule hizi ni vile vya kiada ambavyo huwa vichache kiasi ambacho havitoshelezi wajifunzaji kusoma na kuielewa lugha vizuri. Vitabu vya ziada visipotiliwa mkazo katika shule za sekondari na hata za msingi hupunguza kasi ya ujifunzaji wa Kiswahili, kwani uhimizaji wa usomaji wa vitabu hivyo husaidia wajifunzaji kuimudu lugha ya Kiswahili vizuri.

Mashaka (2015) anaeleza chanzo cha makosa ya udondoshaji na upachikaji wa sauti kama vile /h/ ni kwamba katika lugha ya Kijita hakuna sauti ya /h/, hali hii husababisha wengi wa wanafunzi wanaojifunza kiswahili kutamka na kuandika maneno yenye sauti hii kwa kuidondosha au kuipachika pasipostahili. Kutokana na utafiti wa Mashaka (keshatajwa) ni dhahiri kwamba

mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili kama lugha yake ya pili huweza kutumia sauti za lugha yake ya kwanza katika lugha ya Kiswahili iwapo sauti hizo hazipatikani katika lugha yao ya kwanza. Anaendelea kusema kuwa mwalimu kutojua lugha ya Kiswahili vizuri hupelekea kukwamisha lengo la mawasiliano kwa sababu watu ambao hawajui lugha vizuri wanapozungumza wakati mwingine hutamka maneno yasiyo sahihi hali ambapo husababisha wanafunzi kufanya makosa hayo katika kazi zao andishi. Ufundishaji mbaya wa lugha ya pili hutokana na mwalimu hukosa umilisi na ujuzi wa kiisimu pamoja na mbinu mbalimbali za ufundishaji wa lugha ya pili (kiswahili). Mwanafunzi hujifunza lugha kwa kusikia mwalimu wake anavyozungumza hivyo, mwanafunzi anaposikia matamshi mabaya kutoka kwa mwalimu wake jinsi anavyotamka maneno hayo, naye hufanya makosa yayohayo bila kujua.

Amos (2019) alionyesha kuwa makosa ya udondoshaji wa vokali hutokea kwa sababu lugha ya Kiswahili na lugha ya Kisomali zina mfumo tofauti wa silabi, Kiswahili kinatumia silabi wazi ambazo ni silabi zinazoishia kwa irabu (napenda) ilhali Kisomali kinatumia silabi funge ambazo ni silabi zinazoishia kwa konsonanti (napend). Basi wasemaji wa lugha hii ya Kisomali wanahamisha mfumo huo katika matumizi ya lugha ya Kiswahili ambao ni makosa.

Kulingana na nadharia ya Lugha Kati, sababu mojawapo ambayo huenda ilisababisha kuwepo kwa makosa ya udondoshaji wa sauti /l/ miongoni mwa kazi za wanafunzi ni kutokana na mchakato wa ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa Wairimu (2016). Ambapo mwanafunzi huonyesha ithibati ya kuwa ameshika kanuni ya kijumla lakini hajui ni lini kanuni hiyo haitumiki na pia makosa haya ya ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa huonyesha ni mambo yepi mengine ambayo mwanafunzi hajapata kujifundisha. Wairimu (keshatajwa) anasema kuwa katika Kiswahili sanifu kuna kanuni ya udondoshaji ambapo katika baadhi ya maneno sauti za irabu au konsonanti hudondoshwa ingawa kuna mipaka au sheria ambayo huzingatiwa katika kanuni hii kama vile

huwa tunasema “walimu” badala ya “waalimu”. Wanafunzi wanaojifunza lugha wasipozingatia sheria hizi huwapelekea kufanya makosa.

Wanafunzi huhamisha misamiati kutoka lugha yao ya kwanza na kuitumia katika lugha ya pili kwa sababu wanafunzi hawa hawana umilisi wa lugha ya pili, kulingana na Akoth (2014). Aidha, anasema kuwa wanafunzi hawa wanaposhindwa kupata msamiati mwafaka katika Kiswahili, wao huamua kutumia msamiati wa lugha ya kwanza ili kukidhi mahitaji yao katika matumizi ya lugha ya pili.

Kutokana na maelezo ya watafiti hawa utafiti huu uliweza kueleza vyanzo mbalimbali vya makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili katika Gatuzi dogo la Butula.

2.4 Mikakati ya Kutatua Makosa ya Kisarufi

Ili kupunguza makosa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, Obara (2014) anapendekeza kuwa walimu watumie mtazamo wa uchanganuzi linganuzi katika kulinganua lugha zinazohusika. Itakuwa rahisi kutambua ugumu ambao wanafunzi wanakabiliana nao. Ikiwa mwalimu atatambua vipengele vya lugha vinavyomtatiza mwanafunzi, anaweza kumwelekeza mwanafunzi jinsi ya kutatua ugumu aliyo nao. Mwanafunzi anafaa kuelewa kuwa lugha hutofautiana kiisimu, kwa hivyo wasifikirie kwanza katika lugha yao ya kwanza ndiyo watafsiri kwenda lugha lengwa. Wanafunzi wanafaa kujifunga katika lugha ya Kiswahili na kufuata kanuni zake. Anaendelea kusema kuwa wanafunzi wahimizwe kutumia Kiswahili sanifu wanapowasiliana kwa sababu lugha ya mazungumzo inaathiri mno lugha andishi, hivyo kuna uwezekano kuwa wakijieleza barabara katika mazungumzo huenda wakapunguza makosa yanayojitokeza katika insha zao.

Obara (2014) anapendekeza walimu nao watumie maelezo na alama mahsusi za usahihishaji wa insha. Mara nyingi wanafunzi hawaelewi wanapofanya kosa, kwa sababu kazi husahihishwa bila alama au maelezo ya kumwelekeza mwanafunzi. Ni muhimu mwalimu kuwa na njia mwafaka ya kukosoa insha za wanafunzi. Mathalani, ikiwa kosa ni la kisarufi lipigiwe vijistari viwili chini yake na lile la tahajia lipigiwe kijistari kimoja. Kisha mwalimu anafaa kuwaelekeza wanafunzi kujua ni makosa yepi ya sarufi na ni yepi ya tahajia. Pia anafaa kutoa marejeleo ya vitabu vinavyoshughulikia vipengele vinavyowatatiza wanafunzi. Anatoa maoni kuwa mwalimu anastahili kurudia dhana ambazo wanafunzi hawakuelewa vyema. Uchanganuzi makosa utamfaa mwalimu kwa sababu atajua vipengele vya lugha ambavyo vinastahili kutiliwa mkazo kulingana na uzito wa makosa na kuamua ni vipi vitashughulikiwa. Urudiaji huu wa kufunza vipengele vinavyowatatiza wanafunzi huwasaidia kuwa na umilisi wa lugha ufaao katika lugha.

Katika utafiti wake Obara (keshatajwa) anapendekeza walimu waweze kuweka msingi thabiti kuanzia madarasa ya chini ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na umilisi mwafaka wa lugha ya Kiswahili mapema. Msingi bora wa fonimu utawawezesha wanafunzi kuelewa tofauti iliyoko kifonimu baina ya lugha mbili na hili litawawezesha kuimudu lugha hii mapema. Isitoshe, upungufu na ukosefu wa vifaa bora vya mafunzo huchangia makosa haya, kwa hivyo alipendekeza kuwepo na vifaa vya kutosha vya kufunzia wanafunzi. Aidha, wakuza mitaala hawazingatii kuwepo kwa lugha tofauti nchini Kenya. Wao huchukulia kuwa lugha zote ni sawa na wanaojifunza L2 hutatizika sawa. Mitaala inakosa kuonyesha tofauti za kiisimu kati ya lugha asilia na jinsi inavyoathiri ujifunzaji lugha ya pili, ni vyema ikiwa mitaala itabainisha tofauti hizi na athari za kila lugha asilia katika ujifunzaji wa L2.

Kwa mujibu wa Zakiyyatul, M.H.A na wenzake (2025), kielelezo mwafaka cha ufunzaji wa lugha kinahitajika. Aidha wameongezea kwamba, mwalimu anafaa kuwa kielelezo bora katika matumizi

ya lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, walimu wanahimizwa kupiga msasa lugha yao maadam makosa wanayoyafanya huigwa na wanafunzi wao. Regula. (2015) aidha amesisitiza swala la matamshi. Anasema, mwalimu hafai kuathirika na lugha yake ya kwanza anapotamka maneno katika lugha ya pili. Kazi za waandishi hawa ni muhimu kwa utafiti huu kwa kuwa wametaja dhima ya mwalimu katika shughuli nzima ya ufunzaji wa lugha. Aidha, wamependekeza kuwa matatizo ya walimu yasipuuzwe na vilevile wawe kielelezo bora. Kwa hivyo mwalimu kuwa kielelezo bora ni jambo ambalo limesisitizwa na wataalamu hawa katika matamshi na matumizi mwafaka ya sauti pia ni nguzo muhimu katika utafiti huu.

Zipo njia zilizopendekezwa na Mashaka (2015) kwenye tasnifu yake, za kuondoa makosa ya kisarufi kwa wanafunzi wa Kiswahili. Anasema kuwa watoto wafundishwe lugha ya Kiswahili tangia utotoni ili kuwajengea mawasiliano na maandishi kama nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia inavyosisitiza uhusiano kati ya watu. Kwa wazazi au walezi wahamasishwe ili waweze kutumia lugha ya Kiswahili katika kuwasiliana na wana wao na kuondoa imani potovu kuwa mtoto anapojifunza lugha ya Kiswahili ndiyo chanzo cha kupoteza utamaduni wao. Mashaka (keshatajwa) anaongezea kuwa wanafunzi wanastahili kuelekezwa juu ya utamkaji sahihi wa maneno ya Kiswahili. Matamshi bora katika mawasiliano huleta uhusiano baina ya miundo ya lugha na mawasiliano. Walimu wa Kiswahili wanapaswa kuwajibika katika kufundisha Kiswahili ambapo wanapaswa kujitolea kuwasaidia wanafunzi wao katika Kiswahili ili kuondoa makosa ya kisarufi katika kazi zao pamoja na matamshi.

Ili kuondoa makosa ya kisarufi, Sarah (2018) alipendekeza kwamba walimu wapewe mafunzo ya kutosha juu ya methodolojia mbalimbali za kufundisha Kiswahili kama L2. Anaendelea kusema kuwa kuwe na vifaa vya kutosha vya kufundishia Kiswahili kama L2 kama vile vitabu, picha, vitu halisi na michoro mbalimbali inayohusiana na mada zinazofundishwa ili kumsaidia mjifunzaji

kuimudu lugha hiyo kwa urahisi. Halikadhalika, Sarah (2018) anapendekeza zaidi kuwa serikali isaidie kuwepo kwa mchanganyiko wa walimu na wanafunzi ambao si wazawa wa lugha moja kama vile walimu na wanafunzi wote kuwa wazawa wa lugha ya Kiiraki katika eneo hilo. Aidha, anasema kuwa suala hili linaweza kufanyika kwa kuchagua wanafunzi kutoka maeneo mengine kwenda kusoma katika shule za msingi na sekondari za eneo hilo na walimu kutoka maeneo mengine ili kuhamasisha matumizi ya Kiswahili.

Walimu kuelewa umuhimu wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wao ili waweze kuyapunguza makosa hayo ni jambo ambalo lilipendekezwa na Ntawiyanga (2015). Ntawiyanga (keshatajwa) anaeleza kuwa baadhi ya walimu hawaelewi nafasi ya makosa katika ufundishaji wao. Ni vyema watilie mkazo nafasi ya mwanafunzi katika kuyatambua makosa anayoyafanya na yale yanayofanywa na wanafunzi wenzake ili kuweza kujisahihisha mwenyewe na kuyasahihisha makosa ya wengine. Hivyo, walimu wanastahili kuzingatia kwa kuyachunguza na kuyaeleza makosa yanayofanywa na wanafunzi ndiyo njia bora ya kupunguza makosa hayo.

Kuwekea mkazo shughuli za upangaji wa semina na makongamano katika shule nyingi ambapo Kiswahili hufundishwa kama somo la lazima ni pendekezo katika tasnifu ya Ntawiyanga (keshatajwa) ili kupunguza makosa katika kazi za wanafunzi. Anasema kuwa shughuli hizi zinaweza kuwashirikisha walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili, wataalamu mbalimbali wa isimu na lugha na wadau wengine ili kubadilishana tajiriba zao kuhusu masuala muhimu yaliyopo katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, mbali na kupanga masomo ya muda mfupi kwa walimu wanaofundisha lugha ya Kiswahili, makongamano hayo yatasaidia pia katika kuandaa michezo ya kuigiza, mijadala na midahalo kwa ajili ya wanafunzi wa Kiswahili katika shule mbalimbali ili kuwasaidia kukuza uwezo wao katika lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu ulifaidika kutokana na mapendekezo haya ili kutoa mikakati na mbinu zinazoweza kutumiwa kupunguza makosa katika ujifunzaji na ufunzaji wa Kiswahili.

2.5 Muhtasari

Sehemu hii imehakiki maandishi ya tafiti za awali na kufafanua nadharia ya uchanganuzi makosa. Imeonyesha kuwa kuna umuhimu wa kutambua makosa ya kisarufi katika kiwango cha sauti, maumbo, miundo na maana yanayotokea katika insha za wanafunzi na pana haja ya kutatua makosa hayo ili yasirudiwe mbeleni. Pia sehemu hii imehakiki vyanzo vya makosa hayo na kugundua kuwa mengi yanatokana na athari ya lugha ya kwanza kulingana na kazi za wataalamu katika sehemu hii. Kisha sehemu hii imehakiki mikakati ya kukabiliana na hali hii kulingana na wataalamu mbalimbali. Hata hivyo, uhakiki huo umeonyesha dhahiri kuwa suala la makosa katika insha za wanafunzi ni jambo ambalo linaweza kuzuilika.

SURA YA TATU

MUUNDO WA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sehemu hii inashughulikia muundo wa utafiti kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: kundi lengwa, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, utegemevu na uamilifu wa data na maadili ya utafiti.

3.1 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ni wa mkabala wa kiuthamano. Utafiti wa kithamano unaeleza na unachanganua maandishi kama yanavyopatikana katika usaili. Marshall (1996) anasema kuwa, utafiti wa kithamano ni bora zaidi kutokana na sifa yake ya kushughulikia masuala kwa undani zaidi. Mkabala wa kithamano ulikuwa muhimu kwa utafiti huu kwa kueleza suala la uchanganuzi makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi wanaotumia mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula. Kutokana na mkabala huu utafiti ulihusisha muundo wa usoroveya elezi. Simiyu (2001), anasema kuwa muundo huu hulenga kufafanua sifa za kundi fulani kwa kutumia sampuli iliyoteuliwa kuwakilisha umma lengwa pia huchunguza jinsi mambo yanavyotendeka, sababu za kutendeka kwake na kiasi cha utendekaji. Kombo na Tromp (2006), wanasema kuwa muundo huu hutumiwa kupata data kuhusu mielekeo, maoni, mazoea na pia mambo muhimu yanayohusu elimu na masuala ya jamii. Muundo wa usoroveya elezi ulihusisha kuchanganua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi. Muundo huu ulifaa kwa sababu kundi lengwa ni wanafunzi na walimu ambao ni wengi kiidadi na wana sifa tofauti. Muundo wa usoroveya elezi huhusisha mbinu za ukusanyaji wa data kama vile hojaji, majaribio, kuhoji na kutazama. Muundo wa usoroveya elezi ulifaa utafiti huu kwa kuchunguza makosa ya kisarufi yanayodhihirika katika insha za wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi wanaojifunza Kiswahili,

kueleza chanzo cha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha yao ya pili na kupendekeza mbinu zinazoweza kutumiwa kupunguza makosa haya.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Gatuzi dogo la Butula, Gatuzi la Busia nchini kenya. (Tazama kiambatisho V) Gatuzi dogo hili limepakana na Gatuzi la Kakamega upande wa kaskazini, Gatuzi dogo la Nambale upande wa magharibi, Gatuzi la Siaya upande wa mashariki na Gatuzi dogo la Funyula upande wa kusini. Mtafiti alichagua eneo la Gatuzi dogo la Butula kwa sababu alilifahamu vyema. Tuckman (1988) anasema kuwa wakati mwingine, uzoefu wa eneo la utafiti humpa mtafiti kibali miongoni mwa wakazi wa eneo husika. Wazo hili linatiliwa nguvu na Anol. (2012) anapochangia kuwa, eneo linalofaa kwa utafiti ni lile linalofikiwa kwa urahisi na mtafiti na linaloweza kukubali mwingiliano kati ya mtafiti na wahojiwa.

3.3 Kundi lengwa

Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Bryman 2004, Kombo na Tromp, 2006, Kothari 2008). Utafiti huu ulilenga walimu 72 na wanafunzi 1100 wa Kiswahili wazungumzaji wa Kimarachi wa gredi ya sita katika shule 72 za msingi wanaotumia mtaala wa elimu ya umilisi Gatuzi dogo la Butula ambao ndio huandika insha na wana umilisi kuhusu somo la Kiswahili.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia usampulishaji wa kimaksudi, usampulishaji wa kitabakishi na usampulishaji wa kinasibu. Kombo na Tromp (2006) wanasema jambo la msingi ni kuanza na idadi kubwa na kadri utafiti unavyoendelea, mtafiti atabaki na idadi husika ya utafiti ambayo hasa data zitakusanywa. Sampuli ya asilimia 30 ya wahojiwa ni wakilishi ya kutosha kukusanya data ya kutegemewa na isiyo na upendeleo wowote mradi imeteuliwa kwa misingi ya sifa bainifu za

sampuli, Tuckman (1988). Hivyo basi utafiti huu uliwalenga wanafunzi 330 (asilimia 30 ya wanafunzi 1100) wa gredi ya sita katika shule 22 za kutwa (asilimia 30 ya shule 72 za kutwa). Walimu 22 (asilimia 30 ya walimu 72) wanaofundisha Kiswahili katika gredi ya sita walihusishwa katika utafiti huu. Haingewezekana kuhusisha wanafunzi wote 1100 kwa sababu ya ukubwa wa idadi.

Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika kuchagua shule za kutwa za msingi, wanafunzi na walimu wa kiswahili walioshirikishwa katika utafiti huu kutoka kila shule. Wanafunzi kutoka shule za kutwa walichaguliwa kwa sababu wanafunzi wa shule hizo hutoka katika eneo la utafiti lenye wasemaji wa lahaja ya Kimarachi. Wanafunzi wa gredi ya sita walichaguliwa kwa sababu ni katika gredi ya sita ndipo wanafunzi katika shule nyingi huanza kuandika insha kwa mtihani na pia inatarajiwa kuwa wanafunzi hawa wana umilisi komavu wa lugha ya Kiswahili. Isitoshe kulingana na mtaala mpya wa elimu ya umilisi wanafunzi wa gredi ya mwisho katika shule ya msingi ni wa gredi ya sita. Walimu wa Kiswahili walihusishwa kimaksudi kwa sababu ni wao wanaofundisha somo la Kiswahili na walisaidia katika kusahisha insha za wanafunzi wakibainisha makosa. Simiyu (2001) anaeleza usampulishaji wa kimaksudi kuwa ni mbinu ambayo humpa mtafiti uhuru wa kuteua kimaksudi sampuli anayotaka kwa ajili ya kukidhi malengo ya utafiti wake.

Mbinu ya usampulishaji wa kitabakishi ilitumika kugawa shule katika makundi kama vile shule za wasichana za kutwa (SWK), shule za wavulana za kutwa (SVK) na shule za mseto za kutwa (SMK). Creswell (2012) anaeleza kuwa usampulishaji wa kitabakishi ni mtindo wa usampulishaji wa kiidadi ambapo mtafiti hugawa kundi lengwa katika vikundi kulingana na mambo kama vile jinsia kisha atafanya usampulishaji kwa kutumia usampulishaji wa kinasibu. Utafiti huu ulihusisha shule za mseto za kutwa (SMK) pekee kwa sababu katika Gatuzi dogo la Butula hakuna shule za

wasichana za kutwa na za wavulana za kutwa pekee, zilizoko za jinsia moja ni za kutwa-bweni ambazo hazikulengwa katika utafiti huu. Hii iligundulika baada ya mtafiti kufika nyanjani.

Usampulishaji nasibu ulitumika katika kuchagua wanafunzi waliohusishwa. Kwa mujibu wa Ruane (2005) usampulishaji nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua mshiriki yeyote katika kundi lengwa huwa kubwa.

3.5 Ukusanyaji wa data

Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani kwa hivyo ulihusisha data msingi. Data ilikusanywa na kuchanganuliwa kisha ripoti kuandaliwa kwa njia ya maelezo. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), ukusanyaji wa data unahusu kukusanya taarifa mahsusi zilizokusudiwa kutoa au kupinga uhalisia wa mambo fulani.

3.5.1 Mbinu za ukusanyaji data

Mbinu ya hojaji, usaili, uchunzaji na uchanganuzi wa nyaraka data zilikusanywa kutoka kwa sampuli iliyoteuliwa na majumuisho kufanywa kutokana na matokeo ya data hizo. (Dawson 2002 na Kothari 2008) wameeleza mbinu za ukusanyaji data kama zana au njia atakazotumia mtafiti katika ukusanyaji data. Mbinu na njia zifuatazo zilitumika katika kusanya data.

3.5.1.1 Ujazaji wa Hojaji

Hojaji ilitumika kusanya data kutoka kwa wanafunzi wa shule zilizoteuliwa kwa utafiti huu baada ya kupata idhini kutoka kwa walimu wakuu, hojaji zilikuwa na maswali funge na wazi (tazama kiambatisho I). Wanafunzi wa gredi ya sita walipewa hojaji wazijaze katika shule zilizoteuliwa. Baada ya kujaza Mtafiti alizikusanya na kuziweka kwa shughuli ya uchanganuzi baadaye. Data iliyotokana na hojaji ilimsaidia mtafiti kuchanganua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi.

Mbinu hii ilitumika ili kuwapa watafitiwa fursa ya kutafakari kwa kina kabla ya kujaza hajaji yake. (Oso na Onen 2005) wanasema kuwa hojaji ni maswali ambayo mtafiti huwauliza wasailiwa.

3.5.1.2 Usaili

Utafiti huu uliwasaili walimu wa Kiswahili mmoja baada ya mwingine ili kutambua chanzo cha makosa ya kisarufi, maswali hayo yalikuwa ya aina moja na katika mpangilio ulio sawa (tazama kiambatisho II). Mtafiti aliandaa maswali yanayolenga kukusanya taarifa za aina moja kwa kila kundi la watafitiwa ambao walikuwa walimu waliokuwa wakifundisha shule za msingi za kutwa za Gatuzi dogo la Butula. Maswali hayo yalijibiwa kwa njia ya mdomo na kurekodiwa katika kinasa sauti, na pia kuyaandika kwenye daftari la kumbukumbu. Mbinu hii iliruhusu utoaji wa ufafanuzi pale ilipoonekana taarifa fulani haijaeleweka vyema wakati wa kuuliza maswali kwa wasailiwa na hata kuweka bayana istilahi ambazo zilionekana hazieleweki. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), usaili ni bora kuliko hojaji kwa sababu msaili anaweza kujiweka katika hali halisi ya msailiwa na hivyo kupata data bora zaidi.

3.5.1.3 Uchunzaji

Utafiti wetu ulitumia njia ya uchunzaji katika mazingira ya shuleni kupitia kwa kutangamana kwa mtafiti na wanafunzi pamoja na walimu ili kukadiria chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi wa shule za msingi. Wanafunzi teule walipewa insha kuandika wakisimamiwa na mtafiti aliyeshuhudia jinsi wanafunzi waliandika insha na kuhakikisha kwamba kila mwanafunzi anaandika insha bila kuangalia kazi ya mwenzake wala kuangalia vitabu vyovyote. Mbinu hii vilevile ilitumika kuchunguza nyenzo zilizopo na matumizi yake katika ufunzaji wa insha katika shule zilizoteuliwa. Uchunzaji ulitumika ili kupata habari kwa kuhusisha tajriba na maarifa bila kuuliza watafitiwa maswali yoyote. Uchunzaji ulifanyika katika miktadha ya ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili ili kuchunguza na kubaini chanzo cha makosa ya kisarufi

(tazama kiambatisho III). Kupitia kwa mbinu hii mtafiti alitambua lugha ya mtagusano iliyopo baina ya walimu na wanafunzi. Kulingana na Oso na Onen (2005) uchunzaji ni ushuhudiaji wa tukio linapotendeka na kukusanya taarifa zake. Anaendelea kusema kuwa uchunzaji ni kitendo cha kuchunguza watafitiwa wanafanya nini badala ya kuwauliza maswali.

3.5.1.4 Uchanganuzi wa Nyaraka

Matini kuhusu insha za wanafunzi zilifanyiwa uchanganuzi kubaini makosa ya Kisarufi. Mbinu hii ilitumika kwa kutambua na kudondoa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi katika shule za msingi za kutwa zinazotumia mtaala wa elimu ya umilisi. Kupitia kwa mbinu hii mtafiti alibaini viwango mbalimbali vya makosa ya kisarufi vilivyojitokeza katika insha za wanafunzi wa shule za msingi. Mtafiti alichanganua nyaraka ambazo zilikuwa muhimu na zilizohusiana moja kwa moja na mada ya utafiti. Mtafiti alitembelea afisi ya mtihani katika shule za msingi na idara ya Kiswahili ili kupata idadi kamili ya wanafunzi wa gredi ya sita na idadi ya walimu wa kiswahili. Kutokana na Sarantakosa (2005) anasema uchanganuzi wa nyaraka husaidia kujaliza au kuthibitisha njia nyingine za utafiti.

3.5.2 Vifaa vya Ukusanyaji Data

Kwa kawaida utafiti wowote lazima uwe na vifaa vya kukusanyia data. Creswell (2014) anaeleza kuwa kabla ya kwenda nyanjani kukusanya data, ni sharti mtafiti awe na mpangilio wa vifaa vya kukusanyia data. Anasema kuwa iwapo mtafiti atatumia uchunzaji kukusanyia data sharti awe na mwongozo wa uchunzaji. Utafiti huu ulitumia vifaa vifuatavyo vya ukusanyaji wa data.

3.5.2.1 Hojaji

Hojaji ya mwanafunzi ililenga kukusanya data kuhusu chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha. Hojaji zilitolewa kwa wanafunzi wa gredi ya sita walioteuliwa katika shule za msingi za kutwa zinazotumia mtaala wa elimu ya umilisi katika kaunti ndogo ya Butula. Kwa mujibu wa Paul na

Philip (2024), hojaji ni mkusanyiko wa maswali ambayo yametungwa na hupewa mtu ili ayajibu kwa kuandika. Maswali haya hutungwa kwa mantiki fulani ili kumwezesha mtafiti kupata data anayohitaji. Hojaji zilikuwa na maswali funge na wazi. Maswali funge yalikuwa na muundo maalumu ili kumpa mtafiti nafasi ya kupata majibu yasiyo na maelezo ya ndani. Maswali wazi yalimpa mtafiti uwezo wa kupata data yenye undani kuhusu maswala ya utafiti kama vile chanzo cha makosa ya kisarufi na mikakati ya kutatua makosa hayo katika insha za wanafunzi.

3.5.2.2 Mwongozo wa Usaili

Walimu wa Kiswahili walisailiwa ili kutambua chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi. Mwongozo wa usaili kwa mwalimu wa Kiswahili ulizingatiwa ili kutambua tajriba na viwango vya kuhitimu vya mwalimu kulingana na mtaala wa elimu ya umilisi, pamoja na uwezo wake wa kutambua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wake. Kifaa hiki kilitumika mtafiti alipojiweka katika hali halisi ya msailiwa na hivyo kupata data bora zaidi. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), usaili ni bora kuliko hojaji kwa sababu msaili anaweza kujiweka katika hali halisi ya msailiwa na hivyo kupata data bora zaidi. Mahojiano yalimsaidia mtafiti kupambanua maswala ya utafiti yenye utata hivyo kumwezesha msailiwa kutoa majibu sahihi yaliyo na uwazi. Walimu wa Kiswahili walihojiwa kwa kutumia mahojiano ya maswali funge na mahojiano ya maswali wazi baada ya utazamaji. Hii ilimwezesha mtafiti kulinganisha majibu hayo na aliyoyaona katika ufunzaji na ujifunzaji wa insha na pia yale wanafunzi waliyoyajibu darasani.

3.5.2.3 Orodha ya Uchunzaji

Kifaa hiki kilitumika katika kutambua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi na kutambua chanzo cha makosa hayo. Baada ya wanafunzi walioteuliwa kuandika insha, mtafiti alizisahihisha akidondoa makosa ya kisarufi yaliyojitokeza katika insha hizo. Mtafiti alitazama mbinu na nyenzo alizotumia mwalimu kufundishia darasani na lugha ya mtagusano baina ya wanafunzi na walimu

huku akiongozwa na orodha ya uchunzaji. Kutokana na Gweyi (2014), orodha ya uchunzaji ni kifaa ambacho hutumiwa kunakili tabia na matukio ya watafitiwa nyanjani. Kifaa hiki kilitumika katika mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji wa insha.

3.5.2.4 Mwongozo wa Uchanganuzi wa Nyaraka

Ili kupata data iliyohusiana na makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi, mtafiti aliandaa insha mbili zenye mada “Siku nzuri maishani” na “Rafiki nimpendaye” tazama (kiambatisho IV). Wanafunzi walioteuliwa walistahili kuandika insha moja yazo kwa maneno yasiyopungua mia mbili kwa muda wa dakika arobaini. Kupitia kwa mwongozo wa uchanganuzi wa nyaraka mtafiti alisoma insha za wanafunzi moja baada ya nyingine akibainisha makosa ya kisarufi kwa kuyapigia mstari. Baada ya kuyapigia makosa hayo mistari mtafiti aliyadondoa na kuyapanga kulingana na aina yake.

3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data ya utafiti huu iliwekwa katika misimbo, kupangwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kithamano na pia Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii (SPSS). Utafiti huu ulizingatia uchanganuzi wa kidhamira ambao ni mojawapo wa mbinu za uchanganuzi wa kithamano. Kulingana na Grbich (2012), uchanganuzi wa kithamano ni mchakato wa ugawaji katika vipande, uainishaji na uhusishaji wa vipengele vya data ya ufasili. Mathews na Ross (2010), wanasema kuwa katika kufasiri data kwa kutumia uchanganuzi wa dhamira, maneno au maelezo ya watafitiwa yanawekwa pamoja na ya watafitiwa wenzao ili kumsaidia mtafiti kufafanua data, kutafuta uhusiano baina ya sehemu mbalimbali za data na kueleza mlingano katika mahusiano dhahiri. Kwa mujibu wa Mathews na Ross (2010), maswali elekezi katika uchanganuzi wa dhamira ni kile kilichosemwa na watafitiwa, kwa nini huenda wakasema hayo na huenda wakamaanisha

nini kwa kusema hayo? Maswali haya huwa aminifu katika kutoa mwongozo wa kina kuhusu data ya takwimu.

Katika uchanganuzi wa data kutoka kwa insha tuliongozwa na hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Mtafiti alikusanya sampuli za data za insha alizozipata nyanjani. Pili, ilikuwa kusahihisha insha hizo akitambua makosa ya kisarufi yaliyofanywa na wanafunzi. Tatu, mtafiti aliainisha aina ya makosa ya kisarufi na kuyaweka katika kategoria zake. Kila aina ya makosa ya kisarufi ilipangwa na kuwasilishwa katika majedwali. Vilevile jinsia iliyodhihirisha viwango vikubwa vya makosa ilionyeshwa. Hali kadhalika chanzo cha makosa kilielezwa kulingana na aina ya kosa husika kwa vielelezo vya chati na grafu.

Hatua ya pili, data kutoka kwa hojaji zilizokuwa na maswali wazi zilipangwa katika dhamira na kuwasilishwa kwa unukuzi wa semi mbalimbali katika vielelezo vya chati na grafu. Data hii ilisaidia kueleza waziwazi majibu ya washiriki katika maswali funge. Katika utafiti huu, data kutoka kwa maswali wazi ililinganishwa miongoni mwa watafitiwa, kuainishwa na kisha kufasiriwa. Maelezo yaliyohusiana na data ya kitakwimu yalikusanywa katika hojaji za maswali funge na kuripotiwa kidondoo na hivyo kuweka wazi matokeo.

Hatua ya tatu, uchanganuzi wa data ya kithamano hatua ya kwanza ilikuwa ni baada ya kuzirekodi na kuzinakili rekodi hizo zote kwa kipakatalishi. Baada ya kunakili kwa kipakatalishi, mtafiti alipitia data hiyo na kisha kuichanganua kutegemea madhumuni ya utafiti. Pale alipohitaji unukuzi wa moja kwa moja wa maoni ya watafitiwa, dondoo zilichukuliwa kutoka kwa data iliyochapishwa kwenye kipakatalishi. Maswali elekezi (Nini kilisemwa na watafitiwa, kwa nini huenda wakasema hayo na huenda wakamaanisha nini kwa kusema hayo?), ambayo Mathews na Ross (2010) wanazua yalikuwa mwongozo muhimu katika kupanga data na kuichanganua ili kuhakikisha kwamba kauli za watafitiwa zimezingatiwa mintarafu muktadha wa utafiti.

Mtafiti alilinganisha matokeo ya uchunzaji, hojaji na mwongozo wa usaili ili kutambua chanzo cha makosa ya kisarufi na mikakati ya kutatua makosa hayo katika insha za wanafunzi wa Kiswahili. Uchanganuzi huu ulilenga kudhihirisha uhalali wa matokeo ya utafiti. Hatua hii ilichangia katika mahitimisho na kutoa majibu kwa maswali ya utafiti. Hitimisho la jumla lilifanywa kwa misingi ya data yote iliyokusanywa kupitia kwa vifaa vyote vya utafiti na kuwasilishwa kwa vielelezo vya jedwali, chati na grafu.

3.7 Utegemevu na Uaminifu wa Data

Ili kupima utegemevu wa vifaa vya utafiti, mtafiti alifanya majaribio maradufu katika shule mbili tofauti baada ya mtafiti kupata kibali cha utafiti ili kufanya utafiti. Kwa mujibu wa Patton (2002), “njia moja maarufu ya kubaini utegemevu wa vifaa vya utafiti ni kwa kutumia mbinu ya jaribio maradufu. Majaribio mawili yalifanywa lakini kwa awamu mbili tofauti na kwa wakati tofauti yakihusisha wahojiwa wale wale. Majaribio mawili yalifanyiwa vifaa vya utafiti kwa wakati tofauti kwa walimu watatu na wanafunzi watatu wa Kiswahili wa gredi ya sita katika shule za msingi za kutwa zinazotumia mtaala wa elimu ya umilisi. Majaribio haya yalifanywa katika eneo tofauti na eneo husika la utafiti halisi. Patton (keshatajwa) anaeleza kuwa utegemevu wa vifaa vya utafiti ni ule uwezo wa vifaa vya utafiti wa kutoa matokeo sawa katika majaribio mawili au zaidi kwa kutumia wahojiwa sawa. Matokeo ya jaribio la kwanza na la pili yalikuwa sawa ishara kwamba vifaa vyetu vya utafiti vilikuwa na utegemevu na uaminifu wa kiwango cha juu na vikategemewa kutoa matokeo ya kuaminika katika utafiti wenyewe.

3.8 Maadili ya Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu mtafiti alizingatia maadili ya taaluma kwa watafitiwa ili kutoa taarifa za kweli na za kuaminika bila ya woga wowote. Kwa kuzingatia maadili ya utafiti, utafiti huu ulikwepa changamoto zozote za kimaadili ambazo zingeweza kutokea wakati wa utafiti.

Kabla ya kwenda nyanjani, mtafiti alitafuta kibali kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI) kupitia kwa barua aliyopewa na Kurugenzi la Shahada za upeo za Chuo Kikuu cha MMUST ili kupata idhini ya kusanya data kutoka kwa watafitiwa katika Gatuzi dogo la Butula. Kibali hiki kilipatikana kupitia kwa usajili wa kimtandao. Baada ya kupata kibali cha NACOSTI, mtafiti alikwenda katika Afisa za Utafiti za Gatuzi zilizoko Gatuzi la Busia ili kupata kibali cha kufanya utafiti katika Gatuzi la Busia. Baada ya kupata kibali cha utafiti katika Gatuzi la Busia alienda katika afisi ya Kamishna wa Gatuzi dogo la Butula kupata kibali kingine cha utafiti katika shule za Gatuzi dogo la Butula. Mtafiti alipewa vibali vya kufanya utafiti katika shule husika za msingi za kutwa na walimu wakuu wa shule hizo.

Mtafiti alizingatia usiri wa data ya watafitiwa ili kupata hakikisho kwamba habari walizotoa zisiwekwe hadharani kwa yule ambaye hakushiriki moja kwa moja katika utafiti huu. Ili kuhakikisha usiri kwa mtafitiwa katika utafiti huu, mtafiti aliwahakikishia watafitiwa kwamba habari zote ambazo walitoa zilikuwa za kufaulisha utafiti huu pekee na data ambazo walitoa zilihifadhiwa kwa siri kubwa. Abelson, Frey na Gregg (2004), wanasema sababu kubwa inayochangia majina ya watafitiwa kufichwa ni kwamba inawapa uhuru wa kuelezea wanachohisi na kufikiri bila kuwa na uoga wowote. Katika utafiti huu watafitiwa watahimizwa kuandika insha, kujaza hojaji na kushiriki katika usaili bila uoga wowote. Mtafiti atadondoa kipengele cha majina ya watafitiwa katika hojaji na kutumia herufi kwa minajili ya kuficha majina yao.

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2007), ulinzi wa data ni muhimu katika utafiti wowote ule. Ulinzi wa data unahusisha kanuni ya uchakataji habari za kibinafsi kama vile nyaraka zilizowekwa kama rekodi na datatepe. Katika utafiti huu data ghafi ya Insha, hojaji, usaili na uchunzaji ilihifadhiwa katika kipakatalishi kilicho na nywila iliyofahamika na mtafiti pekee yake. Washiriki

wote walipewa msimbo wa nambari uliotumika kujumuisha na kupanga data zote zilizofuatia. Mtafiti alipanga data aliyokusanya kwa minajili ya kuiwasilisha.

Ulinzi wa saikolojia ya watafitiwa ulihusisha kuuliza maswali ambayo hayakukwaza watafitiwa kuhusu utamaduni wao, aliuliza maswali kwa namna ambayo haingezua uchungu au majuto ya mambo yaliyotendeka na pia kuhakikisha kwamba hakuna utamaduni wa mtu yeyote unadhalilishwa. Ulinzi huu ulizingatiwa katika hojaji na usaili.

3.9 Muhtasari

Sura hii inaangazia njia na mbinu za utafiti ambazo zinahusisha muundo wa utafiti, kundi lengwa, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data, utegemevu na uaminifu wa data na maadili ya utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

4.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia uwasilishaji na uchanganuzi wa data kuhusu makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa mtaala wa umilisi katika Gatuzi la Busia. Matokeo yamewasilishwa katika sehemu tatu kulingana na madhumuni ya utafiti.

4.1 Makosa ya Kisarufi

Madhumuni ya kwanza yalikuwa kubainisha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa mtaala wa umilisi katika Gatuzi la Busia. Matokeo yalibaini makosa yafuatayo;

Neno la Kiswahili	**Neno la kimarachi**	**Athari**	**Kiambatisho**
Mtu	Mundu	Mutu	VII
Hisabati	Isabu	Isabati	VIII
Mkristo	Mukirisito	Mkiristo	XIII

Jedwali hili linaonyesha mifano ya maneno ya Kiswahili na Kimarachi. Jedwali linadhihirisha kwamba makosa mengi yalitokana na uhamishaji wa muundo wa lugha ya Kimarachi hadi kwa Kiswahili pasi kufahamu kuwa lugha hizi mbili zinatofautiana kimuundo.

4.1.1 Makosa ya Sarufi Sauti (fonolojia)

Kutokana na data tuliyokusanya, wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa umilisi walifanya makosa ya udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti, uyeyushaji wa sauti na ubadilishanaji wa sauti katika insha zao.

4.1.1.1 Udondoshaji wa sauti

Makosa ya udondoshaji yalijitokeza katika insha za watafitiwa. Kulingana na data yetu makosa hayo yalifanywa kutegemea sauti ambayo ilifuatana na sauti husika. Massamba (2016) anaeleza kwamba udondoshaji ni utaratibu wa kutoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai na kishazi. Kuainisha makosa katika kategoria mbalimbali ni hatua ya tatu ya kuchanganua makosa kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa Corder (1974). Kwa hivyo utafiti huu uliainisha makosa ya udondoshaji wa sauti kwa misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili wa gredi ya sita wa mtaala wa elimu ya umilisi katika Jamii ya Wamarachi. Ilibainika kwamba yapo makosa ya udondoshaji wa sauti /w/a/h/ na /i/ ambayo yalijitokeza kama yanavyofafanuliwa katika kipengele kinachofuata.

4.1.1.1 .1 Udondoshaji wa sauti /w/

Neno sahihi	**Neno lenye athari**	**Kiambatisho**
Alikuwa	Aliku^a	VII
Huwa	Hu^a	VIII
Mweupe	M^eupe	XVII
Waliweka	Wali^eka	VII
Tuliweka	Tuli^eka	VII

Jedwali 1 udondoshaji wa sauti /w/

Kutokana na jedwali 1, sauti /w/ imedondoshwa pale ambapo imefuatwa na irabu kama vile katika neno [hu^a]. Kutokana na data yetu makosa mengi ya udondoshaji wa sauti /w/ yalitokea wakati sauti hiyo inatokea katikati ya irabu mbili kama vile: (aliku^a badala ya alikuwa, hu^a badala ya

huwa). Matokeo haya yanaoana na mawazo ya Amos (2019) ambaye alitambua kwamba sauti /w/ ilidondolewa na vilevile kuchopekwa katikati pale ambapo irabu mbili zilifuatana.

4.1.1.1.2 Udondoshaji wa sauti /a/

Neno sahihi	**Neno lenye athari**	**Kiambatisho**
Wakati	Wak^ti	XIII
Nilimpata	Nilimp^ta	XIII
Nikavaa	Nikava^	VII
Baada	Ba^da	VII
Aliandaa	Aliand^a	VII

Jedwali 2 Udondoshaji wa sauti /a/

Jedwali 2 linaonyesha kuwa vokali /a/ imedondoshwa katika mazingira ya katikati ya konsonanti mbili na mwishoni mwa neno baada ya konsonanti. Udondoshaji wa sauti ulipofanywa na mwanafunzi ulibadilisha maana ambayo mwanafunzi alilenga kuwasilisha. Kwa mfano, mwanafunzi alilenga kusema, “Anapenda masomo” akaishia kusema, “Anapend msomo”. Amos [2019] kwenye tasnifu yake anaeleza vokali /a/ inaachwa wakati inapopatikana mwishoni mwa neno huku ikifuatwa na konsonanti. Anaendelea kusema kuwa makosa haya hufanyika kutokana na hali kwamba Kiswahili na lugha ya Kisomali zina mfumo tofauti wa silabi, Kiswahili kinatumia silabi wazi ilhali Kisomali kinatumia silabi funge. Katika utafiti huu lugha ya Kiswahili na ya Kimarachi zote zinatumia silabi wazi ila makosa haya yalitokana na hali kwamba wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi wangali wanajifunza Kiswahili ndio inawapelekea kufanya makosa husika.

4.1.1.1.3 Udondoshaji wa sauti /h/

Neno sahihi	Neno lenye athari.	Kiambatisho
Hisabati	^isabati	VIII
Huonekana	^uonekana	XII
Huheshimu	Hu^eshimu	XVI
uhusiano	U^usiano	XIV
Hakuna	^Akuna	VII
Hapo	^apo	VII

Jedwali 3: Udondoshaji wa /h/

Jedwali 3 linaonyesha kuwa sauti /h/ imedondoshwa zaidi mwanzoni mwa maneno na katika mazingira mengine katikati mwa maneno kama katika neno [hu^eshimu]. Kutokana na data yetu, sauti /h/ ilidondoshwa kwa mazingira ya kufuatiwa na irabu. Matokeo haya yanaungwa mkono na mawazo ya Mashaka (2015) ambaye aligundua udondoshaji wa /h/ katika lugha ya Kijita. Hali hii hutokana na ukosefu wa sauti hiyo katika lugha ya kwanza. Pia iwapo mwanafunzi bado anajifunza Kiswahili. Utafiti huu umebaini kuwa katika lugha ya Kimarachi, hakuna sauti /h/ hali hii inasababisha wengi kutamka na kuandika maneno yenye sauti hii kwa kuidondosha au kupachika pasipostahili hasa miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili huchanganyikiwa na kukosa kujua waitumie sauti hiyo wapi.

4.1.1.1.4 Udondoshaji wa sauti /i/

Neno sahihi	Neno lenye athari	Kiambatisho
Wasichana	Was^chana	XIV
Alipita	Alip^ta	VIII
Hutimiza	Hutim^za	IX
Ilitua	Il^tua	XII
Havijawai	Hav^jawai	XII

Jedwali 4: Udondoshaji wa /i/

Katika jedwali 4 hili sauti /i/ inaonekana kudondoshwa inapotokea katikati ya sauti mbili za konsonanti. Hali hii inalingana na maoni ya Amos (2019) anayeeleza kwamba vokali /i/ hudondoshwa inapotokea katikati ya konsonanti mbili na baada ya konsonanti. Katika neno nilimp^ta konsonanti mbili zinazorejelewa ni /p/ na /t/. Wanafunzi wa gredi ya sita wazungumzaji wa Kimarachi walishindwa kujua ni wakati upi watumie sauti /i/ na ni wakati upi wasiitumie jambo ambalo liliwapelekea kufanya makosa.

4.1.1.2 Makosa ya Uyeyeshaji

Neno sahihi	Neno lenye athari.	Kiambatisho
Vyema	v̲iema	XVI
Vyakula	v̲iakula	XVII
Mpya	mp̲ia	IX
Mwaka	M̲uaka	XI
Kwenda	K̲uenda	XII

Jedwali 5: Uyeyushaji wa sauti /y/ na /w/

Jedwali 5 linadhihirisha wazi kwamba wanafunzi walikosa kuyeyusha irabu /i/ ili kupata kiyeyusho /y/ kama vile neno [viatu] pia wakakosea kuyeyusha irabu /u/ ili kupata kiyeyusho /w/ mfano neno [kuenda]. Maoni haya yanaungwa mkono na utafiti wa Obara (2014) ambaye aligundua kwamba wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusi walishindwa kuyeyusha maneno yaliyokuwa na mfuatano wa irabu ambayo yalihitaji kuyeyushwa. Wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi walishindwa kujua ni wakati upi irabu zikifuatana zilistahili kuyeyushwa. Hali ambayo iliwapelekea kufanya makosa katika insha zao. Kwa hivyo wanafunzi wa gredi ya sita wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wajifunzaji wa Kiswahili hufanya makosa ya uyeyushaji wakati kunatokea mfwatano wa irabu mbili tofauti ambapo irabu ya kwanza kwa mfwatano huo inastahili kuyeyushwa. Wanafunzi hao hawatambui wakati upi wanastahili kuyeyusha sauti na wakati upi wasiyeyushe sauti.

4.1.1.3 Uchopekaji wa Sauti.

Katika mchakato huu tulibainisha makosa ya kisarufi, herufi zilichopekwa katika maneno ya lugha ya Kiswahili, mwanzo, kati na mwishoni mwa neno. Al-Khresheh (2016) anafafanua akirejelea Nadharia ya Uchanganuzi Makosa kuwa makosa ya mwanafunzi yanastahili kuainishwa na kufafanuliwa kama vile uchopekaji wa sauti katika utafiti huu. Sauti mbalimbali za lugha ya Kiswahili zimechopekwa katika insha za watafitiwa kama ifuatavyo:

4.1.1.3.1 Uchopekaji wa sauti /u/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Mtu	M**u**tu	VII
mchwa	M**u**chwa	VIII
Mnapenda	m**u**napenda	XIII
Mna	M**u**na	XVI
Kuwa	K**u**wa	XVI
Mswaki	M**u**swaki	VII

Jedwali 6: Uchopekeji wa sauti /u/

Jedwali 6 linaonyesha jinsi sauti /u/ imeongezwa katikati ya neno hasa maneno yenye sauti mwambatano kama vile katika neno [mutu] /m/ ni sauti mwambatano ambayo inachopekwa sauti /u/ kimakosa. Mchakato huu unafanana na maoni ya Ontieri (2018) ambaye alionyesha jinsi sauti /u/ ilichopekwa katikati ya konsonanti mbili wakati konsonanti tangulizi ikiwa kama silabi funge. Uchopekaji huu ulivuruga usanifu wa maneno na lugha ya kiswahili. Kutokana na utafiti huu hali hii ilitokana na sababu kwamba wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa umilisi hawatambui silabi funge kwa hivyo hawajui wakati upi irabu inaongezwa kwenye konsonanti na ni wakati upi isiongezwe.

4.1.1.3.2 Uchopekaji wa sauti /i/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Mkristo	Mk**i**risto	XIII
Insha	In**i**sha	X
Askari	As**i**kari	XIV
Alfajiri	Al**i**fajiri	VIII
Ardhi	Ar**i**dhi	XIV

Jedwali 7: Uchopekeji wa sauti /i/

Jedwali 7 linaonyesha uchopekaji wa irabu /i/ sawia na irabu /u/, irabu /i/ ilichopekwa katikati ya sauti mwambatano na vilevile katikati ya maneno yenye asili ya kigeni kama vile katika neno [asikari]. Hali ii inaoana na maoni ya Nyagah (2016), katika tasnifu yake alitambua kuwa wanafunzi wazungumzaji wa Kitigania waliongezea sauti /i/ kwenye maneno yaliyo na sauti mwambatano na hujitokeza zaidi kwa maneno yaliyokopwa. Alitambua kuwa makosa haya yanatokana na athari ya kugha ya Kitigania iliyo na muundo tofauti wa silabi na lugha ya kiswahili. Anaendelea kusema inawezekana kosa hili likatokana na mkakati wa kujifunza lugha ya pili hasa wanafunzi wanapojaribu kusahilisha miundo ya lugha ya pili. Kutokana na utafiti huu hakuna muundo wa silabi funge katika lugha ya Kimarachi hali hii inachangia wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi kuchopeka sauti /i/ katika baadhi ya meneno na kusababisha makosa.

4.1.1.4 Ubadilishaji wa sauti

Utafiti wetu ulibaini kuwa baadhi ya sauti za Kiswahili hupitia mageuzi na kudhihirisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wasemaji wa Kimarachi. Corder (1967) kwenye Nadharia yake ya Uchanganuzi Makosa, anaeleza kwamba makosa mengi ya wajifunzaji wa lugha ya pili yanatokana na wajifunzaji wenyewe kutumia kimakosa kanuni za lugha ya pili wanayojifunza. Watafitiwa walitumia sauti mahali pasipofaa na neno husika kupoteza maana aliyokusudia kuwasilisha. Watafitiwa walitumia sauti mbadala kwa njia ifuatayo.

4.1.1.4.1 Matumizi ya /i/ badala ya /a/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Nilijifunza	Nilijifunz**i**	XIII
Hupenda	Hupend**i**	XIV
Anapenda	Anapend**i**	XVII
Ujasiri	Uj**i**siri	XVII
Kusaidia	Kusaidi**i**	XIV

Jedwali 8: Matumizi ya sauti /i/ badala ya /a/

Kutokana na jedwali 8 wanafunzi wametumia sauti /i/ badala ya /a/ katika maneno. Ubadilishaji huu umejitokeza mwishoni na katikati mwa neno hasa inapotokea baada ya konsonanti. Amos (2019) kwenye tasnifu yake alionyesha jinsi wanafunzi wa Kisomali walifanya makosa ya kubadilishana sauti za irabu anaonyesha kuwa sauti /a/ inawakilishwa na sauti /e/, /i/, /o/ na /u/. Vilevile wanafunzi wa Kimarachi walifanya makosa ya ubadilishanaji wa /a/ kuwa /i/ kutokana na ukosefu wao wa umilisi wa lugha ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu ni wazi kwamba wanafunzi wa gedi ya sita wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wajifunzaji wa Kiswahili hawana umilisi wa kutosha wa lugha ya Kiswahili hali ambayo inasababisha makosa ya ubadala wa sauti.

4.1.1.4.2 Matumizi ya sauti /i/ badala ya /u/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Anaupenda	Ana**i**penda	XV
Vile ulivyo	Vile **i**livyo	XV
Kutumia	Kut**i**mia	X
Ugonjwa ukaisha	Ugonjwa **i**kaisha	XV
Uliimbwa	**I**liimbwa	XIV

Jedwali 9: Matumizi ya sauti /i/ badala ya /u/

Jedwali 9 linaonyesha mageuzi ya irabu /u/ kuwa /i/ mwanzoni mwa neno kama vile [ugonjwa **i**kaisha] na katikati mwa neno kama vile [ana**i**penda]. Maoni haya yanaoana na utafiti wa Amos (keshatajwa) aliyeonyesha jinsi wanafunzi wa Kisomali walibadilisha matumizi ya sauti za vokali na kusababisha makosa katika Kiswahili. Wanafunzi wa Kimarachi walibadilisha matumizi ya sauti /i/ badala ya /u/ kutokana na hali kuwa walishindwa kutambua miundo na matumizi ya ngeli ya U-I jambo ambalo liliwapelekea kufanya makosa katika insha zao. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaeleza kwamba wajifunzaji wa lugha husika hufanya makosa kutokana na kutoelewa miundo ya lugha ya pili. Kwa hivyo wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi kutokana na hali ya kutoelewa miundo ya lugha ya Kiswahili kulileta makosa ya matumizi ya sauti /i/ badala ya /u/.

4.1.1.4.3 Matumizi ya sauti /y/ badala ya /l/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Jina lao	Jina **y**ao	XIV
Jina la	Jina **y**a	XIV
Soma la	Somo **y**a	XV
Eneo la	Eneo ya	X
Kanisa la	Kanisa **y**a	XVI

Jedwali 10: Matumizi ya sauti /y/ badala ya /l/

Jedwali 10 linadhihirisha sauti /y/ imetumika mwanzoni mwa neno badala ya sauti /l/ kama vile katika neno [**y**ao]. Kutokana na data yetu sauti /y/ imetumika kwa mazingira ya sauti /l/ inapofwatiwa na irabu. Maoni ya Mashaka (2015) yanakaribiana na utafiti huu, katika tasnifu yake amebaini kwamba baadhi wa wazungumzaji wa lugha ya Kijita hutumia fonimu /r/ badala ya /l/. Anasema kuwa katika lugha ya Kijita ambayo ndiyo lugha yenye wasemaji wengi Musoma hawana herufi ya /l/ bali wana herufi ya /r/ tu. Kwa sababu hiyo wanafunzi wengi wa jamii ya Kijita hukanganyika wasijuwe jinsi ya kutumia fonimu hizi mbili ipasavyo. Vilevile katika Lugha

ya Kimarachi sauti /l/ haipo ilhali kunayo sauti /y/ hali ambayo inafanya wanafunzi wachanganyikiwe wasijue wapi watumie sauti /l/ na wapi wasiitumie.

4.1.1.4.4 Matumizi ya sauti /y/ badala ya /w/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Mwili wake	Mwili yake	XV
Mpira wa	Mpira ya	XV
Ukarimu wake	Ukarimu yake	XV
Masomo ya	Masomo wa	XV

Jedwali 11: Matumizi ya sauti /y/ badala ya /w/

Kutokana na jedwali 11 sauti /y/ imetumika kimakosa badala ya sauti /w/ mwanzoni mwa neno. Makosa haya yamejitokeza hasa katika upatanisho wa kisarufi katika maneno yenye ngeli ya U-I kama vile [mpira ya]. Makosa haya yanatokana na hali kwamba wanafunzi wa gredi ya sita wazungumzaji wa Kimarachi wanashindwa kuelewa ni wakati upi watumie sauti /y/ badala ya /w/ na wakati upi sauti /w/ itumiwe. Athari ya lugha ya Kimarachi kwa Kiswahili imechangia uwepo wa makosa haya. Makosa haya hujitokeza mwanzoni mwa neno, sauti za maneno katika ya ngeli ya U-I katika umoja hubadilishana kimatumizi na kusababisha makosa.

4.1.1.4.5 Matumizi ya sauti /th/ badala ya /dh/

Neno sahihi	**Neno lenye athari.**	**Kiambatisho**
Wanaadhibiwa	Wanaa**th**ibiwa	XIII
Riadha	Ria**th**a	IX
Nidhamu	Ni**th**amu	XVI
Kunidhalilisha	Kuni**th**alilisha	XI
Wanidhalimu	Wani**th**alimu	XI

Jedwali 12: Matumizi ya sauti /th/ badala ya /dh/

Kutokana na data yetu sauti /th/ imetumika kwa mazingira ya sauti /dh/ inapofwatiwa na irabu. Sawia na Amos (2019) ambaye anadai kuwa wasemaji wa lugha ya Kisomali wanaotumia lugha ya Kiswahili, walitumia / th / pale ambapo wanakusudia kutumia / dh /. Lugha ya Kiswahili ina fonimu hizi mbili /dh/ na /th/ lakini lugha ya Kisomali ina fonimu /dh /. Wasemaji hawa walitumia /dh/ badala ya /th/ kwa sababu hawajui ni wapi inatumika na ni wapi haitumiki katika lugha ya pili. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inaeleza kuwa mwanafunzi anaposhindwa kuelewa matumizi ya lugha ya pili bila shaka husababisha makosa katika matumizi ya lugha ya pili. Vilevile katika utafiti huu wanafunzi wasemaji wa Kimarachi walishindwa kutumia sauti /dh/ na kutumia /th/ katika maneno yenye sauti /dh/ kutokana na sababu kuwa hawakuelewa ni wapi sauti hiyo hutumika na wapi haitumiki.

Utafiti huu unahitimisha kwamba wanafunzi wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wajifunzaji wa Kiswahili hufanya makosa ya sauti kama vile; udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti, uyeyushaji wa sauti na ubadilishanaji wa sauti. Uanishaji huu unaungwa mkono na maoni ya Sirdhar (1981) katika Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ambaye anaeleza kuwa makosa ya wajifunzaji lugha huwa ya aina nyingi. Tofauti za kimuundo za lugha ya Kimarachi na Kiswahili Pamoja na umilisi finyu wa wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi wanaojifunza Kiswahili ulichangia wanafunzi kufanya makosa haya. Kwa hivyo walimu wanastahili kutilia mkazo miundo za lugha ya Kiswahili vilevile kuboresha umilisi wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi.

4.1.2 Makosa ya Sarufi Maumbo (mofolojia)

Kulingana na matokeo ya data tuliyokusanya wanafunzi wa gredi ya sita wazungumzaji wa Kimarachi wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi walifanya makosa katika maumbo ya maneno ya Kiswahili. Makosa haya yalijitokeza katika insha walizoziandika kama ifuatavyo.

4.1.2.1 Kutenganisha neno visivyo

Neno sahihi	**Neno lenye athari**	**Kiambatisho**
Anajipenda	Ana—jipenda	IX
Tunapofanya	Tunapo—fanya	IX
Hupenda	Hu—penda	XV
Hunifunza	Huni—funza	XV
Kuwakataza	Kuwa—kataza	XIV

Jedwali 13: Kutenganisha neno visivyo

Jedwali 13 linaonyesha kwamba maneno yametenganishwa mara mbili kimakosa. Maneno ambayo yametenganishwa ni vitenzi ambavyo vimeongezewa viambishi mwanzoni kabla ya mzizi kama vile [tunapo—fanya]. Kemunto (2017) kwenye Tasnifu yake ana maoni sawa, anasema kuwa wanafunzi wengi hutatizika na maneno yaliyo marefu sana kiasi cha kufikiria kulitenganisha ili yawe mawili au zaidi. Mbaabu (1995) anasema kuwa umbo la neno ambalo hutenganishwa huwa na mzizi wa vitenzi. Kabla ya mzizi huo viungo kadha wa kadha kama vile viambishi, na viungo vya wakati hutumiwa. Wanafunzi walifanya makosa ya kutenganisha maneno kutokana na hali kuwa hawakuelewa misamiati ipi inastahili kutenganishwa na ipi haistahili kutenganishwa.

4.1.2.2 Kuunganisha neno visivyo

Neno sahihi	Neno lenye athari	Kiambatisho
Wa darasa	Wa/darasa	XI
Wa kiume	Wa/kiume	X
Wa kike	Wa/kike	X
Kaka wawili	Kaka/wawili	VIII
Kwake vitabu	Kwake/vitabu	VIII

Jedwali 14: Kuunganisha neno visivyo

Kutokana na jedwali wanafunzi wameunganisha maneno mawili na kuyafanya kuwa kama neno moja. Maneno ambayo yameunganishwa ni kihusishi + nomino kama vile [wa/darasa] na nomino + kivumishi [kaka/wawili]. Kemunto (2017) sawa na utafiti huu anasema kuwa mofimu mbalimbali za Kiswahili kuna zile hujisimamia na zile hazijisimamii. Katika tasnifu yake Kemunto (Keshatajwa) wanafunzi waliunganisha mofimu ambazo hujisimamia zenyewe kama vile nomino + kivumishi, nomino + kiunganishi, nomino + kihusishi na kitenzi + kielezi. Uunganishaji huu ulisababisha makosa katika maneno ya Kiswahili kutokana na hali kuwa wanafunzi walishindwa kutambua maneno yapi yanastahili kuunganishwa na yapi hayastahili kuunganishwa.

4.1.2.3 Kuacha silabi katika neno

Neno sahihi	Neno lenye athari	Kiambatisho
Wanyama	Wanya^	IX
Uhusiano	U^sianao	XVI
Wali	Wa^	X
Mmoja	M^ja	X
Ninaenda	^nenda	XV

Jedwali 15: Kuacha silabi katika neno

Jedwali limedhihirisha kuwa wanafunzi waliwacha silabi mwishoni mwa neno kama vile [Wanya^] katikati mwa neno [u^siano] na mwanzoni mwa neno [^nenda]. Maoni ya Kemunto (2017) yanaunga mkono utafiti huu anaposema kwamba wanafunzi huacha silabi katika maandishi ya maneno fulani kutokana na upungufu wa umilisi wa viambishi katika Kiswahili. Kuandika kwa haraka kwa mwanafunzi vilevile huchangia kuacha silabi katika neno na husababisha makosa katika neno husika. Hali hii ilishuhudiwa katika wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi katika uandishi wa insha zao.

Utafiti huu unahitimisha kuwa wanafunzi wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi hufanya makosa ya kimaumbo katika lugha ya Kiswahili. Makosa hayo ni kama vile; kutenganisha na kuunganisha neno visivyofaa na kudondoa viambishi katika neno. Makosa haya hutokana na uandishi wao kwa haraka na vilevile kutokuwa na umilisi mpana wa viambishi. Kwa hivyo wanafunzi hawa wanastahili kusoma vitabu vingi ili kuwa na ufahamu mpana wa viambishi pia wafanye mazoezi mengi ya kuandika insha ili kuepukana na makosa haya.

4.1.3 Makosa ya sarufi miundo (sintaksia)

Makosa ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi

Sentensi sahihi	**Sentensi yenye athari**	**Kiambatisho**
Anaupenda mwili wake	Ana**i**penda mwili **y**ake	XV
Ana meno meupe	Ana meno **ny**eupe	XIV
Ana baba mmoja na mama mmoja	Ana baba **m**oja na mama **m**oja	XIV
Eneo la Butula	Eneo **ya** Butula	X

Jedwali 16: Makosa ya upatanisho wa kisarufi katika sentensi

Jedwali 16 linaonyesha sentensi ambazo si sanifu kutokana na upatanisho wa kisarufi ambao wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi hawakuzingatia. Sawa na utafiti huu, Obara (2014) anasema kuwa katika Kiswahili sanifu Ngeli ya nomino huathiri upatanisho wa viwakilishi, vivumishi na vitenzi katika sentensi. Wanafunzi walishindwa kupatanisha viambishi vinavyofaa katika maneno katika sentensi kupekelea makosa katika sentensi hizo. Mwanafunzi aliandika (meno nyeupe) badala ya (meno meupe) inaonyesha kuwa mwanafunzi huyo hatambui kuwa katika maneno ya ngeli ya LI-YA, kiambishi (me-) hupatanishwa kama kiambishi tangulizi katika sentensi hali ya wingi. Utafiti huu unahitimisha kuwa wanafunzi wa gredi ya sita wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wanaojifunza Kiswahili hufanya makosa ya upatanisho wa kisarufi kutokana na upungufu wao wa umilisi wa viambishi na matumizi ya ngeli. Kwa hivyo walimu wao wanastahili kutilia maanani ufunzaji wa viambishi na ngeli na matumizi yake.

4.1.4 Makosa ya sarufi maana (semantiki)

Makosa ya kisemantiki yalidhihirika katika insha za wanafunzi wazungumzaji wa kimarachi. Wanafunzi walifanya makosa haya ambapo sentensi ilikosa kutoa maana iliyokusudiwa. Makosa ambayo wanafunzi walifanya ni kama yafuatayo:

4.1.4.1 Matumizi ya msamiati usiofaa

Sentensi sahihi	**Sentensi yenye athari**	**Kiambatisho**
Yeye hufanya vyema katika mtihani	Yeye **hunga** vyema katika mtihani	X
Yeye ni mweupe pepepe	Yeye ni mweupe **tititi**	XIV
Yeye si mnene wala mkonde	Yeye si **mnono** wala mkonde	X
Tuliabiri gari	**Tulipanda** gari	VII

Jedwali 17: Matumizi ya msamiati usiofaa

Kutokana na jedwali 17, maneno yanayokaribiana kimaana yametumiwa katika sentensi lakini kisemantiki hayafai katika muktadha husika. Kama vile neno (tulipanda) katika sentensi "tulipanda gari" mwanafunzi ametumia neno hili badala ya (tuliabiri). Katika Nadharia ya Sarufi Zalishi, Chomsky (1957), anadai kuwa mwanafunzi atatumia ujuzi alionao katika lugha asilia kujieleza katika lugha lengwa. Hali hii ni sawia na utafiti huu ambapo wanafunzi walitumia ujuzi wa lugha ya Kiamarachi katika kujieleza katika lugha ya Kiswahili. Hali hii ilizua makosa ya kisemantiki katika insha za wanafunzi.

4.1.4.2 Mrundiko wa maneno katika sentensi

Sentensi sahihi	**Sentensi yenye athari**	**Kiambatisho**
Yeye si mrefu wala mfupi	Yeye si mrefu wala **si** mfupi	XIII
Walemavu na maskini	Walemavu na **wenye ni** maskini	XIV
Hupenda kucheza kandanda na kusoma hadithi	Hupenda kucheza **mchezo wa** kandanda **pia yeye hupenda** kusoma hadithi	XVI
Watoto na watu ambao wanamshinda umri	Watoto **pia** na watu ambao wanamshinda umri	XVI

Jedwali 18: Mrundiko wa maneno katika sentensi

Jedwali 18 limeonyesha kuwa maneno yasiyokuwa na maana katika sentensi kulingana na muktadha yameongezwa. Maneno haya yanastahili kuondolewa katika sentensi ndiposa sentensi hiyo itoe maana iliyokusudiwa. Kama vile katika sentensi (*Yeye si mrefu wala si mfupi) neno **si** limerundikwa kimakosa katika sentensi, neno hilo linastahili kuondolewa katika sentensi ndiposa sentensi hiyo iwe na maana kisemantiki. Kemunto (2017) katika Tasnifu yake sawa na utafiti huu, anasema kuwa mwanafunzi hutumia kiambajengo (nomino, kiwakilishi, kivumishi, kitenzi,

kielezi, kiunganishi, kihusishi na kihisishi) kimakosa katika sentensi. Makosa haya hutokea wakati mwanafunzi hajui mahali mwafaka pa kutumia kiambajengo husika katika sentensi. Huu udhaifu wa mwanafunzi kushindwa kubainisha nafasi na matumizi mwafaka ya viambajengo vya sentensi huhusishwa na lugha ya pili (Kiswahili).


Utafiti huu unahitimisha kuwa wanafunzi wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wajifunzaji wa Kiswahili hufanya makosa ya kisemantiki katika insha zao kama vile; matumizi ya msamiati usiofaa na kurundika maneno yasiyo ya maana katika sentensi kutokana na wingi wao wa msamiati pasi kujua matumizi yake katika sentensi na kulazimisha msamiati huo katika sentensi. Hali hii hupoteza maana katika sentensi. Larsen (1992) anasema Nadharia ya Uchunganuzi Makosa inashikilia kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi hufanya lugha kupoteza maana na isieleweke na msomaji. Hivyo basi kando na wanafunzi kuwa na ukwasi wa msamiati wanastahili kuelewa maana na matumizi ya msamiati huo ili wajue wapi pa kuutumia na wapi hawastahili kuutumia.

4.2 Chanzo cha makosa ya kisarufi

Madhumuni ya pili ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza chanzo cha makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi. Al-Khresheh (2016) anatambua kuwa kufafanua vyanzo vya makosa ni daraja ya nne katika Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Kutokana na hojaji kwa mwanafunzi, kiongozi cha usaili kwa mwalimu na kiongozi cha uchunzaji, maelezo ya chanzo cha makosa ya kisarufi yalitambuliwa. Utafiti huu ulizingatia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ili kuchunguza vyanzo mbalimbali kama vile ifuatavyo;

4.2.1 Kutofahamu wakati wa kutumia na kutotumia sauti /h/

Makosa ya udondoshaji wa sauti hasa udondoshaji wa sauti /h/ ilitokana na sababu kwamba wanafunzi walichanganyikiwa ni wakati upi inafaa kutumiwa na ni wakati upi haifai kutumiwa. Selinker (1972) anakiita ujumlishaji mno wa kanuni za lugha lengwa katika lugha kati. Kwa hivyo, kwa kuwa lugha ya Kiswahili huwa na sauti /h/ wanafunzi huishia kuitumia kiholela inapofwatiwa na irabu. Kutokana na sauti zilizorekodiwa wakati wa ufundishaji wa insha na mwalimu darasani, wanafunzi walishindwa kutambua kuwa wamefanya makosa ya udondoshaji wa sauti /h/. Hali hii inatokana na juhudi za wanafunzi kurahisisha miundo ya lugha lengwa kama mkakati wa mawasiliano.



Kielelezo 1: Kutofahamu wakati wa kutumia na kutotumia sauti /h/

Data katika kielelezo 1 inaonyesha kuwa asilimia 60% ya wanafunzi wazungumzaji wa kimarachi wa gredi ya sita walichopeka sauti /h/ mwanzoni mwa neno, 30% katikati mwa neno na 10% mwishoni mwa neno kwa sababu hawakuelewa ni wakati upi sauti /h/ inastahili kuchopekwa na

wakati upi haistahili kuchopekwa. Ontieri (2018) sawa na utafiti huu anaeleza kuwa ukosefu wa sauti /h/ katika lugha ya Ekegusi huwafanya wazawa wa jamii-lugha husika kutoitumia pale inapostahili kutumiwa. Ukosefu wa sauti /h/ katika lugha ya Kimarachi ilichangia makosa katika insha za wanafunzi.

4.2.2 Athari ya lugha ya Kimarachi


Wanafunzi walidhihirisha makosa ya uchopekaji wa sauti kama vile uchopekaji wa sauti /u/ katika maneno yenye silabi mwambatano. Kwa mafano neno mtu, sauti /u/ ilichopekwa kimakosa na kuwa mutu*. Hali hii ilitokana na athari ya lugha ya Kimarachi iliyo na muundo tofauti wa silabi na lugha ya Kiswahili. Silabi mwambatano haipo katika lugha ya Kimarachi hali hii huwapelekea wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili kuongezea sauti ya irabu palipo na sauti mwambatano. Kama vile katika neno muvulana badala ya mvulana. Inawezekana kosa hili kutokana na mkakati wa kujifunza lugha ya pili hasa wanafunzi wanapojaribu kusahilisha miundo ya lugha ya pili. Makosa haya yamedhihirishwa na insha za wanafunzi ambazo waliziandika.

4.2.3 Mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili

Hii ni sababu nyingine ya wajifunzaji wa Kiswahili wa gredi ya sita wazungumzaji wa Kimarachi kufanya makosa katika insha zao. Kulingana na data iliyokusanywa, iligundulika kwamba ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wa gredi ya sita wa mtaala wa umilisi kwa kiasi kikubwa unaanza rasmi katika mazingira ya shuleni. Huu ni wakati ambao mjifunzaji anakuwa na umri wa miaka kati ya 4-8. Kwa mujibu wa Han (2004) na Gas na Selinker (2008) upo umri fulani ambao mjifunzaji akijifunza lugha anaweza kuimudu kwa kiasi fulani na endapo umri huo utakuwa umevuka ujifunzaji wake utakuwa mgumu na utaambatana na ufanyaji wa makosa. Kwa mujibu wa wataalamu hao huu ni umri ambao upo kati ya miaka 2-10. Kulingana na wataalamu hao, umri

ambao wajifunzaji wanakuwa katika mazingira ya shuleni ambako ndiko wanajifunza Kiswahili zaidi ni umri ambao si rafiki sana kwao kujifunza lugha na kuimudu vizuri. Hii ni kwa sababu lugha ya kwanza inakuwa tayari imeshakomaa kiasi cha kufanya ugumu kuingiza sarufi ya lugha nyingine katika bongo zao. Hii ina maana kwamba umri huo unakuwa umegawanyika kiasi ambacho haumtoshi mjifunzaji kuingiza kiukamilifu kanuni za lugha ya pili anayojifunza.

Hata hivyo, kando na suala la umri kujitokeza katika mazingira ya shuleni, mazingira yenyewe ni tatizo kwa sababu tumegundua kwamba wajifunzaji hao wanaoanza kujifunza Kiswahili katika mazingira ya shuleni hawakitumii Kiswahili hicho kwa kiwango kinachokidhi. Hii ni kwa sababu Kiswahili kinatumika mwalimu anapokuwa darasani tu baada ya hapo wajifunzaji hao wanaendelea kutumia Kimarachi kuwasiliana. Data kutoka kwa hojaji ya mwanafunzi ilibaini kuwa 70% hutumia lugha ya kimarachi kila mahali, 20% wakiwa nyumbani na 10% shuleni. Hali hii inasababisha ugumu kwa wajifunzaji hawa kufahamu kanuni za lugha wanayojifunza kutokana na ufinyu wa matumizi yake. Kwa hivyo, ni wazi kwamba kuanza kujifunza rasmi lugha ya Kiswahili katika mazingira ya shuleni ni changamoto kwa wajifunzaji hawa kuielewa vizuri lugha hiyo.




Kielelezo 2: Mahali pa matumizi ya lugha ya Kiswahili

Kutokana na baagrafu, idadi kubwa ya wajifunzaji wa Kiswahili 70% huzungumza lugha ya Kimarachi kila mahali ikifuatiwa na 20% ikizungumza nyumbani matumizi ya mwisho yakiwa 10% shuleni. Felician (2019) sawa na utafiti huu alibaini kuwa kuna matumizi makubwa ya lugha ya Kihaya katika mazingira ya shuleni Pamoja na nyumbani hali ambayo inachangia makosa ya kisarufi katika ujifunzaji wa lugha Kiswahili.

4.2.4 Mielekeo ya wanafunzi

Kutokana na mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la insha, wanafunzi waliulizwa ikiwa walifurahia somo la insha wakapewa vibadala viwili ili mmoja achague. Vibadala hivi vilikuwa: Ndiyo na La.




Kilelezo 3: Mielekeo ya wanafunzi

Kutokana na kielelezo 3, watafitiwa (72%) walionyesha kuwa na mwelekeo chanya kuhusu somo la insha kwa kuitikia kuwa wao hufurahia kuandika insha. Hunsen (1977) anasema kuwa, wanafunzi wenye mielekeo chanya kuhusu somo hupata alama za juu kuliko wale wenye mielekeo

hasi. Ni matarajio ya mtafiti kuwa mwelekeo huu unafaa kudhihirika kupitia matokeo bora katika mtihani wa insha. Katika kielelezo 3 wanafunzi 28% waliodai kutofurahia somo la insha waliwalaumu walimu kwa kusema kuwa, hawakusahihisha kazi zao mara kwa mara, hawakuwapatia maelezo, walimu mara nyingi walitumia muda wa somo la insha kufunzia vipengele vingine vya lugha kama vile sarufi na fasihi, walimu hawakutumia vifaa vya kidijitali katika ufunzaji kama inavyopendekezwa na elimu ya umilisi.

4.2.5 Maarifa na Kutohitimu kwa walimu

Walimu kutokuwa na maarifa kamili na ujuzi wa kufundisha lugha ya Kiswahili kulionekana kuwa chanzo cha kufanya makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi. Kutokana na usaili kwa walimu 20% ya walimu wanaofundisha gredi ya sita somo la Kiswahili hawajahitimu kama walimu kwa hivyo hawana maarifa na ujuzi wa kufundisha somo hilo. Walimu hawafahamu vizuri kanuni na sheria za lugha wanayofundisha na pia hawana maarifa ya mbinu zinazopaswa kutumika kufundishia Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanalingana na maoni ya Sarah (2018) ambaye anasema kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili ni tofauti na ufundishaji wa kawaida kwa sababu huhitaji maarifa, ujuzi na umilisi wa lugha ya pili inayofundishwa. Aidha, wafundishaji wanatakiwa wawe wamepitia mafunzo maalumu ambayo huwawezesha kuwafundisha wajifunzaji kwa kutumia stadi na mbinu mbalimbali ili waweze kufikia umilisi wa lugha ya pili. Utafiti wetu uligundua kwamba wale walimu ambao hawajahitimu hawana ujuzi wa kutambua makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi ili kuwaelekeza wanafunzi ipasavyo. Hali hii pia imefanya walimu hao kutotambua mbinu nzuri za ufunzaji na ujifunzaji wa insha jambo ambalo huwapelekea wajifunzaji hao kufanya makosa katika insha zao.




Kielelezo 4: Maarifa na Kutohitimu kwa walimu

Chati hii imeonyesha kuwa asilimia 80% ya walimu wanaofundisha Kiswahili ndio waliohitimu kama walimu pekee ilhali asilimia 20% ya walimu wafunzaji Kiswahili hawajahitimu kama walimu. Utafiti huu unakubaliana na maoni ya Sarah (2018) anayesema kwamba walimu wasiohitimu hawafahamu vizuri kanuni na sheria za lugha wanayofundisha na pia hawana maarifa ya mbinu zinazopaswa kutumika kufundishia Kiswahili. Hali hii huwapelekea kutowasaidia wanafunzi katika uandishi wa insha kwa sababu hawana ujuzi na umilisi wa lugha ya Kiswahili.

4.2.6 Matumizi ya Mbinu zisizofaa za ufundishaji

Hojaji kwa mwanafunzi zilibaini kwamba mbinu za ufundishaji wa insha zilichangia katika wanafunzi kufanya makosa katika insha zao. Walimu wengi wanapuuza mbinu ambazo zinafaa kutumika katika ufunzaji wao. Dhima ya mbinu mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili inaungwa mkono na wataalamu wengi Ellis (1997), Lighbown na Spada (1990) na Gathumbi na

Masembe (2005). Ingawa mbinu nyingi zilijadiliwa na baadhi ya hizo kupendekezwa katika ufundishaji wa insha katika sura ya pili. Utafiti huu ulibainisha kuwa nyingi ya mbinu hizi hazitumiki katika ufundishaji wa insha hali ambayo inachangia makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi. Kutokana na data ya hojaji kwa wanafunzi mbinu za makundi, kuandika insha kibinafsi, mhadhara, mjadala na sauti zilizorekodiwa zilitumika katika ufundishaji wa insha ila kwa asilimia ya chini.



Kielelezo 5: Matumizi ya mbinu za ufundishaji


Kutokana na kielelezo 5, 60% ya watafitiwa walisema kuwa mbinu ya makundi inatumiwa mara kwa mara 30% wakasema kuwa mbinu hii inatumiwa wakati mwingine 10% wakasema kuwa mbinu ya makundi haitumiwi kamwe. Mbinu ya kuandika insha kibinafsi; watafitiwa 90% walisema kuwa mbinu hii inatumiwa ilhali 10% ya watafitiwa wakasema kuwa inatumiwa wakati mwingine. Mbinu ya mhadhara; watafitiwa 20% walisema kuwa inatumiwa huku 25% wakisema inatumiwa wakati mwingine na 55% wasema haitumiwi kamwe. Mbinu ya mjadala; watafitiwa

10% walikubali kuwa inatumiwa mara kwa mara 20% wakasema mbinu hii inatumiwa wakati mwingine na 70% wakaonyesha kutotumika kamwe kwa mbinu hii. Mbinu ya sauti zilizorekodiwa; 100% ya watafitiwa walisema kuwa mbinu hii haitumiki kamwe. Matokeo haya yanaonyesha kuwa mbinu za makundi na kuandika kibinafsi ndizo walimu hupendelea kutumia kuliko zile zinazomweka mwanafunzi katika nafasi ya kwendesha ujifunzaji wa insha. Felician (2019) alitambua kuwa matumizi ya mbinu mbaya za ufundishaji wa lugha ya pili humpelekea mjifunzaji wa lugha hiyo kufanya makosa. Anaendelea kusema kuwa walimu kutokuwa na mbinu mbadala ya kufundisha wanafunzi lugha ya pili husababisha wanafunzi wazungumzaji wa Kihaya kufanya makosa katika kazi zao. Maoni haya yanaoana na utafiti huu ambapo utafiti ulitambua kwamba walimu wamejikita sana katika mbinu mbili ambazo hazina mshiko katika kupunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi.

4.2.7 Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia

Hii ni sababu nyingine ya makosa kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wamarachi. Kupitia kiongozi cha uchunzaji na usaili kwa walimu ilibainika kwamba vifaa vya ufundishaji havipatikani shuleni na vile ambavyo vipo havitoshelezi mahitaji ya ufundishaji wa insha. 100% ya watafitiwa walikubali kuwa kunavyo vitabu vya kiada shuleni ingawaje vitabu hivyo havina maelezo zaidi jinsi ya kuandika insha hali ambapo inaonyesha upungufu wa vitabu hivi. Kutokana na usaili kwa walimu, 95% ya watafitiwa walisema kuwa kuna tarakilishi shuleni ambazo zililetwa na sirikali ingawaje 100% ya watafitiwa hawazitumii katika ufundishaji wa insha. 100% ya watafitiwa walieleza kwamba kunavyo vifaa vya kidigitali shuleni ila havitumiki kamwe kwa manufaa ya wanafunzi wajifunzaji wa Kiswahili. Walimu walitoa sababu kadhaa zinazowapelekea wasitumie vifaa vya kidigitali katika ufundishaji wa Kiswahili kama vile:

ukosefu wa umeme shuleni, kutokuwa na fahamu ya matumizi, shule husika imeweka sheria kali ili utumie na kutopata muda wa kuvitumia.




Kielelezo 6: Uwepo na matumizi ya vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji

Baagrafu imeonyesha kuwa asilimia 100% ya watafitiwa walisema kuwa kunavyo vitabu vya kiada shuleni na hakuna aliyesema kuwa vitabu vya kiada havipo shuleni. 95% wakasema kuwa kunazo tarakilishi shuleni huku 5% wakisema kuwa hakuna tarakilishi shuleni. 100% ya watafitiwa walisema kuwa tarikilishi zilizopo shuleni hazitumiki katika ujifunzaji wa insha. 100% ya watafitiwa walisema kwamba hakuna vifaa vya kidigitali shuleni ambavyo vinatumika katika ujifunzaji wa Kiswahili shuleni. Sarah (2018) anaeleza kuwa shule nyingi za vijijini hutumia tu vitabu vya kiada katika ujifunzaji jambo ambalo limesababisha wanafunzi kutokuwa na utafiti mpana wa lugha na kuwapelekea wanafunzi kufanya makosa.

4.2.8 Athari ya lugha ya kwanza

Utafiti ulibaini kuwa wazazi wana mchango wa makosa ya watoto wao katika uandishi wa insha ambao ndio wajifunzaji wa Kiswahili. Elimu ya umilisi inaipa kipaumbele lugha asili, Kimarachi

ikiwa miongoni mwazo. Katika ufundishaji wa insha katika elimu ya mtaala mpya wa umilisi, wazazi wanastahili kusaidia wanao katika mafunzo ya shuleni. Hali hii imesababisha wazazi wasiokuwa na uelewa wa masomo ya shule kuwapotosha wanao na kuwarithisha makosa. Hojaji ya mwanafunzi ilibaini kuwa 90% ya watafitiwa hutumia lugha ya Kimarachi katika mtagusano wao wa nyumbani. Kutokana na utafiti wetu ni vigumu kutumia lugha asili kufundisha lugha ya Kiswahili hasa uandishi wa insha. Kwa hivyo wazazi wanapowapa mwelekeo kuhusu uandishi wa insha idadi kubwa hutumia lugha ya Kimarachi jambo ambalo husababisha makosa wakati wanafunzi wanapoandika insha zao.



Kielelezo 7: Matumizi ya lugha ya kwanza

Chati imeonyesha kuwa, kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili asilimia 90% hutumia lugha ya Kimarachi katika mtagusano wao wa nyumbani huku asilimia 10% ikitumia lugha ya Kiswahili katika mtagusano wao wa nyumbani. Maelezo haya yanaungwa mkono na utafiti wa Sara (2018) ambaye aligundua kwamba lugha ya Kiiraki imeathiri lugha ya Kiswahili kwa kiasi fulani ambapo

wakati mwingine Wairaki wanatumia sauti za lugha yao katika lugha ya Kiswahili. Halikadhalika, muundo wa lugha ya Kiiraki umeathiri lugha ya Kiswahili jambo ambalo linasababisha makosa wanapokuwa wanajifunza Kiswahili.

Al-Khresheh (2016) anaeleza kuwa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inadai kuwa baadhi ya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili hutokana na athari ya lugha ya kwanza. Utafiti huu uligundua kuwa athari ya lugha ya Kimarachi Pamoja na kutofahamu wakati wa kutumia na kutotumia sauti, mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, mielekeo ya wanafunzi, maarifa na kutohitimu kwa walimu, matumizi ya mbinu zisizofaa za ufundishaji na uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia ndivyo vyanzo vya makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wanaojifunza Kiswahili. Kwa hivyo walimu, wanafunzi Pamoja na wazazi wao wanastahili kubuni mbinu za kuepukana na vyanzo hivi.

4.3. Hatua za kutatua makosa ya kisraufi.


Kutokana na data kutoka kwa hojaji kwa mwanafunzi, kiongozi cha usaili kwa mwalimu na utaratibu wa kiongozi cha uchunzaji, njia za kukabiliana na makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa gredi ya sita zilipendekezwa. Utafiti ulipendekeza njia na mbinu mbalimbali ambazo zinastahili kuzingatiwa ili kutatua makosa ya kisarufi ambayo yanafanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili. Utafiti huu ulifuata hatua za Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967), Kulingana na Corder baada ya mwalimu kutambua makosa kisa vyanzo vyake kuchunguzwa, anastahili kutambua mbinu za kushughulikia makosa hayo. Jambo hili litasaidia ili mwanafunzi asiyarudiye makosa hayo. Data ya utafiti ilipendekeza mbinu na njia zifuatazo ili kupunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi.

4.3.1 Uhamasishaji wa wazazi kuhusu Mfumo wa Elimu ya Umilisi

Kutokana na usaili wa walimu wa Kiswahili, 70% ya wasailiwa walipendekeza uhamasishaji wa wazazi kuhusu mfumo wa elimu ya umilisi. Kutokana na mfumo wa elimu ya umilisi ulioanzishwa mwaka 2017, mzazi anastahili kushirikiana na mwanawe kufanya baadhi ya mazoezi ya nyumbani aliyopewa shuleni. Ili mzazi kumpa mwanafunzi mwelekeo unaofaa kuhusu uandishi wa insha sirikali inastahili kuwahamasisha kuhusu elimu ya umilisi. Serikali iwahamasishe wazazi jinsi ya kuwapa wanao mwelekeo masomoni na mchango wao katika masomo hayo kando na kushughulikia maslahi ya wanao. Hali hii itapunguza makosa katika insha za wanafunzi. Mashaka. (2015). Katika tasnifu yake anasema kuwa wazazi wawe vielelezo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili hasa wanapokuwa nyumbani. Hali hii itasaidia sana wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kuwajengea msingi na uwezo zaidi wa kujiamini ambapo ni mojayapo ya umilisi wa kimsingi unaokuzwa na mtaala wa elimu ya umilisi.

4.3.2 Uandishi wa insha

Mtaala wa umilisi unapendekeza mwanafunzi kufanya kazi yake mwenyewe kupitia kwa uelekezi wa mwalimu. Ghodbane. (2010) anaona uandishi wa wanafunzi utakuwa bora ikiwa wanafunzi watatunga na kuandika insha zao wao wenyewe.



Kielelezo 8: Mazoezi ya kuandika insha

Kutokana na data katika hojaji ya wanafunzi; 85% ya watafitiwa walikubali kuwa mazoezi ya kuandika insha mara kwa mara yatapunguza makosa ya kisarufi katika insha. 10% ya watafitiwa walikana kuwa uandishi wa insha mara kwa mara hautapunguza makosa ilhali 5% ya watafitiwa hawakuwa na ufahamu kama uandishi wa insha mara kwa mara utapunguza makosa ya kisarufi katika insha zao. Utafiti huu unapendekeza uandishi wa insha mara kwa mara kwa sababu mwanafunzi atapata kutambua makosa ya kisarufi ambayo anayafanya na kisha kiyarekebisha kupitia kwa uelekezi wa mwalimu.


4.3.3 Kutumia alama sahihi za usahihishaji wa insha

Kutokanana data za uchunzaji na usahishaji wa insha za wanafunzi, Utafiti ulipendekeza matumizi ya alama sahihi za usahihishaji katika insha za wanafunzi. Maarek (2009) anaona kuna umuhimu wa kuonyesha masahihisho kwa kutumia alama sahihi. Maarek (keshatajwa) anasema mirejesho hiyo ndiyo iliyowawezesha watafitiwa (wanafunzi) wake kujikosoa na kuboresha uandishi wao.

Maarek anahimiza walimu kutumia alama za usahihishaji za insha ila utafiti wake hauonyeshi ufunzaji wa hizo alama za usahihishaji kwa wanafunzi. Utafiti huu unapendekeza ufunzaji na matumizi ya alama sahihi za usahihishaji wa insha kwa wanafunzi.

Ganobocsik-Williams (2004) anaona kuwa kwa kuwa ni wajibu wa Asasi za Elimu ya Juu kuwaandaa na kuwaendeleza wanataaluma wake katika ufundishaji wa uandishi, ni vyema kupatiwa msaada wa kifedha na asasi za fedha. Hii itaimarisha ufundishaji na tafiti mbalimbali. Vilevile, itawezesha mikutano ya wanataaluma na kuwezesha ziara ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kujionea programu na mikakati mbalimbali ya uandishi. Pia, suala hili linasisitizwa na Matoti na Shumba (2011). Utafiti wetu unaonelea kuwa walimu wakipigwa msasa vizuri kuhusu uandishi wa insha bila shaka wanafunzi watafaidika kwa kiasi kikubwa kwa sababu wataelekezwa na walimu ambao ni wataalamu.

4.3.4 Kubaini miundo tatanishi



